

# **Kitabu Cha Danieli**

**Na Ndugu Heath Stapleton**

[www.kanisalakristo.com](http://www.kanisalakristo.com)

## UTANGULIZI WA KITABU CHA DANIEL

### I. Utangulizi

- A. Kitabu cha Daniel ni tafsiri ya kitheologia ya Taifa la Yuda wakati wa ukimbizi wa Babeli.
1. Danieli alitaka awasisitizie wasomaji wake waliokuwa uhamishoni kuhusu nguvu na kazi ya Mungu ambayo ilionekana katika matukio ya kihistoria yaliyotokea.
- B. Wakati kilipoandikwa kitabu:
1. Matukio ya kitabu yalitokea kati ya mwaka 606 - 536 K.K.
  2. Sehemu za kitabu hiki kimeandikwa na Danieli; inawezekana kitabu hiki kiliandikwa mwaka wa 536-500 K.K.
- C. Kitabu kiliandikwa wapi?
1. Kama Daniel aliandika baadhi ya nakala basi sehemu kubwa zingeliandikwa uhamishoni.
  2. Na nyingine labda ziliandikwa baada ya kurudi Palestina.
- D. Nani alikusaya maelezo haya?
1. Hajulikani.
  2. Labda Ezra ambaye aliongeza kwenye nakala zilizoandikwa na Daniel katika karne ya 6 K.K.

### II. Yaliyomo

- A. Kitabu hiki ni muunganiko wa simulizi za kihistoria (1-6) pamoja na maono juu ya kuhubiri maafa makubwa (7-12).
- B. Mhusika mkuu ni Daniel.
1. Katika historia ya maisha yake ni sawa na Yusufu.
  2. Maisha yake na kazi yake yalienea muda wote wa miaka 70 ya uhamishoni.
  3. Alikuwa anaheshimika sana katika nyumba ya kifalme na dunia, Dan. 2:48; 5:29; 6:28.
  4. Ilikuwa wakati uleule wa Ezekiel (Eze. 14:14, 20).
  5. Mpendwa sana (Dan. 9:23; 10:11, 10:19).
  6. Alizaliwa kwenye mwaka 620 K.K.
  7. Akiwa na miaka 15 alihamia Babeli.
  8. Maana ya jina lake ni “Mungu ndiye mwamuzi wangu.”
  9. Maono yake yanaonyesha matukio ya baadae, kutoka uhamishoni mpaka Kristo.
  10. Anaelezea matukio kwa usahihi lakini wanafunzi wengine wanajaribu kukana uvuvio na wengine wanasema kuwa kimeandikwa baada ya matukio yote kutendeka, 167 K.K.
- C. Kitabu kina mpangilio fulani unaonyesha kuwa kitabu hiki kina matukio ya uvuvio wa waandishi mbalimbali kuliko kuandikwa na mtu mmoja.

1. 1:1-2:3, Iliandikwa na nafsi ya tatu (3rd Person).
2. 2:4-7:28, Iliandikwa na nafsi ya tatu lakini katika Ki-Arabu.
  - a) Inasadikiwa kuwa sehemu hii yaweza kuwa ilichukuliwa katika vitabu vya historia vya Babeli na Uajemi.
3. Daniel mwenyewe aliandika 8:1-12:13 mtu wa kwanza katika Ki-Ebrania.

### III. Mazingira ya kihistoria

- A. Kitabu kinaanza na kufukuzwa kwa Daniel, Shadraka, Meshaki na Abednego kwenda Babeli mwaka wa tatu wa utawala wa Mfalme Yehoakim, 606 K.K.
  1. Hii ilikuwa mara ya kwanza kati ya tatu ambapo wayahudi walifukuzwa nchini.
- B. Historia kubwa inahusu uhusiano wa Danieli: kwa Nebukadneza, Mfalme wa Babeli na kupiga Yuda.
  1. Inajadili uhusiano wao na jinsi Danieli alivyotumia zawadi kutoka kwa Mungu ili kujenga uhusiano na mfalme kwa uhusiano huu alimsaidia Nebkadneza kutawala jinsi ambavyo Mungu anataka kama mfalme angekuwa na kiburi ndipo Danieli alipoluwa anaitwa kwenda kwa Mfalme.

### IV Ukweli kuhusu Mji wa Babeli

- A. Kutokana na hali yetu ya miji ya sasa, Babeli isingekuwa chochote lakini katika dunia ya kipindi kile ulikuwa mji mkubwa sana. Mji ulikuwa na maili za mraba 15 ukiwa umezungukwa na kuta kubwa urefu ft. 300 upana futi 80 na kushuka chini msingi ulikuwa futi 35. Mji ulikuwa na malango ya shaba - 100 na minala ya ulinzi 250.
- B. Hekalu lilikuwa jengo kubwa zaidi duniani. Mfano wa dhahabu wenye uzito wa 50,000 ratili (pounds).

### V. Maelezo mafupi ya Kitabu cha Danieli / Muhtasari

- A. Danieli anapata nguvu 1:1-20.
- B. Ndoto ya Mfalme inatafsiliwa na Daniel 2:1-49.
- C. Hadithi ya tanuru la Moto 3:1-30.
- D. Ndoto ya pili inatafsiriwa 4:1-37.
- E. Sherehe ya Beshaza na maandiko ya Ukutani 5:1-30.
- F. Danieli katika shimo la simba 5:31-6:28.
- G. Maono ya Danieli na wanyama wanne 7:1-28.
- H. Maono ya Danieli ya Kondoo na Beberu 8:1-27.
- I. Maombi ya Danieli 9:1-23.
- J. Unabii wa majuma sabini 9:24-27.
- K. Maono ya Mungu 10:1-11:1.
- L. Ufunuo wa yajayo 11:2-20.
- M. Kipindi cha Mpinga-Kristo, 11:21-12:3.
- N. Hitimisho, 12:2-13.

### VI. Vifungu vya ufunguo katika Danieli

- A. 1:8.
- B. 1:17.
- C. 2:19-20.
- D. 2:47-48.
- E. 3:3-6.
- F. 3:12.
- G. 3:16-18.
- H. 3:23-25.

- I. 4:1, 3.
- J. 5:25-28.
- K. 5:5.
- L. 6:3-4.
- M. 6:6-7.
- N. 6:10-11.
- O. 6:14-16.
- P. 6:19-21.
- Q. 6:26.
- R. 9:5.
- S. 9:16, 17, 19.

**VII. Faida tunazoweza kupata toka kwenye kitabu hiki ni:**

- A. Kwamba inawezekana kubaki waaminifu kwa Mungu hata wakati wa kipindi kigumu, Efe. 3:20.
- B. Tunapaswa kufahamu kuwa Mungu anafurahia matendo yetu ya kiroho.
- C. Mara kwa mara ni lazima mtu wa Mungu asimama peke yake.
- D. Kwa kila jambo jema shukurani ni kwa Mungu.
- E. Sote tunavyo vipawa tuwezavyo kuvitumia.
- F. Inawezekana kuwa katika nafasi yenye mamlaka makubwa na bado tusipate itilafu.
- G. Mungu atakuwa mshindi katika yote afanyayo.
- H. Tunaweza kuwa na hakika na kujiamini katika maneno ya Mungu.

**Sehemu Ya Pili**

**Maisha Ya Daniel, Hanania, Mishaeli na Azaria**

**Danieli 1**

**I. Uhamisho Wa Kwanza Wa Wayahudi, 1:1-5.**

- A. Uhamisho kwa Babeli ulianza karibu mwaka wa tatu wa Mfalme Yehoyakimu wa Yuda, 606 K.K. 1:1.
  - 1. Ni mwaka ule ule ambao Nebukadneza aliwekwa kuwa Mfalme.
- B. Katika uvamizi wa Hekalu vitu vingi viliibiwa pasipo kuharibiwa, 1:2.
  - 1. Pengine ni vyombo vya dhahabu na fedha vilivyotumiwa na Belishaza kutoka katika hekalu, Dan. 5:1-4.
  - 2. Mnamo mwaka 597 baada ya Babeli kuishambulia Yerusalemu kwa mara ya pili, kwa kuwa Yehoyakimu alijaribu kuasi, waliiba hata zaidi ya vile vilivyohusika na hekalu pamoja na hazina katika Jumba la Kifalme.
- C. Hekalu liliweza kudumu mpaka 586, wakati wa maangamizo ya mwisho ya Yerusalemu chini ya kabila la Yuda.
- D. Uhamisho wa kwanza ulijumuisha vijana wa kiume wa Kiyahudi ama watu waungwana, 1:3-5.
  - 1. Idadi yao kamili haijulikani lakini walitafutwa vijana wote wazuri.
  - 2. Walipelekwa Babeli kwa lengo la kutayarisha uongozi.
    - a. Malazi na Chakula yalikuwa bora.
    - b. Taaluma yao ilikuwa juu.
    - c. Taratibu zao za mafunzo zilikuwa ngumu.
    - d. Waliweza kupita walitayarishwa kwa kazi ya ufalme.
  - 3. Mwalimu Mkuu wa Mafunzo haya alikuwa Ashpnazi "Mkuu wa Balaza."
    - a. Tafsiri nzuri "Mkuu wa Matowashi".
    - b. Kwa namna moja ama nyingine wale waliowekwa kwa huduma hii walifanywa matowashi.

## II. Daniel na Rafiki zake (1:6-21).

- A. Watu pekee waliotajwa katika kundi hili la uhamisho ni Daniel, Hanania, Mishael na Azaria (1:6, 7).
1. Pengine walikuwa wadogo mno katika kipindi hicho, (12-15).
  2. Walipelekwa shule walipewa majina mapya ya Kibabeli.
  3. Alama ya kila jina kwa mwenzake ni ishara ya mamlaka juu yake.
    - a) Mfalme Yehoyakimu, alitwa hivyo na mtawala wa Misri  
 aliyetitwa Farao Necho, jina lake la asili alikuwa Eliakim,  
 2 Fal. 23:24.
    - b) Mfalme Zedekia alipata jina hilo kutoka kwa Nebukadneza, wazazi wake walimwita Matania, 2 Fal. 24:17.
  4. Majina mapya ambayo walipewa Daniel na rafiki zake ni vigumu kuyafasiri.
    - a) Maana ya "Daniel" - "Yahwe ni mhukumu wangu." Jina lake likabadilishwa na kuwa "Beltshaza" lenye kusifia dini ya Babeli. Kwa maana ya "Acha Beli alinde maisha yake."
    - b) Hanania - "Yahwe ni mwenye neema." Lakini jina lake alitwa "Shadraki" lenye kusifia jina la Aku, mungu wa kale wa Sumeri, mungu huyu aliyehusika na mwezi. Jina lake linamaana ya - "Chini ya amri ya Aku."
    - c) "Misheal" maana yake ni "Nani ni kama Mungu?" Meshaki, jina lake jipya lina maana, "Nani ni kama Aku?"
    - d) "Azaria" ina maana ya "Yahwe ameshasaidia." Jina lake likabadilika na kuwa "Abed-nego." Ambalo tena linasifia mungu wa hekima aliyetitwa "Abu" na maana ya Abu ni "mtumishi wa Abu."
- B. Jambo linalojionyesha kati ya watu hawa ni namna yao ya kujifunza tamaduni za Wababeli pasipo kutenda dhambi kutokana na tamaduni hizi za kigeni, 1:8-16.
1. Majina ya Kibabeli yalitumika katika nyakati fulani maalumu, lakini bado walijulikana kwa majina yao ya Kiebrania na historia, Dan. 2:17; 4:8-19; 5:12.
  2. Swala la chakula shuleni halikuwafanya kuwa chanzo cha kumwacha Mungu, walifuata makatazo ya sheria ya Musa na wakawa imara zaidi na wenye hekima zaidi ya watu wote.
- C. Kutokana na hili ni kuonekana kwa matendo ya Mungu kwa yeyote aliyekuwa mwaminifu.

## Daniel 2

### Ndoto Ya Nebukadneza

#### I. Dan. 1:20, Walikuwa wenye hekima katika mambo yote.

- A. Katika sura ya pili inaonyesha upekee wa Daniel na rafiki zake katika baraza la Nebukadneza.
- B. Karibu sasa ni mwaka wa pili katika utawala wa Nebukadneza.
  1. Wababeli walihesabu miaka kinyume na tunavyohesabu sisi, kwa kweli

Daniel na rafiki zake walikuwa katika huduma ya kifalme kwa muda wa miaka mitatu, sasa ni karibu 603 K.K.

## II. Ndoto ya Nebukadneza.

- A. Biblia (kifungu) kinaeleza hapa kwamba mfalme aliota ndoto pengine ilikuwa ni hali ya kawaida inatokea.
1. Ni hali ya kawaida kwamba pindi mtu anapoamka, hawezi kukumbuka kile alichoota.
  2. Hali hiyo ilimfanya kushangaa na ikamkosesha raha kwa vile hakuweza kuelewa maana ya ndoto ile.
    - a) Ilikuwa ni jambo la kawaida kwa watu wa siku zile pengine na baadhi leo kuona kwamba ndoto zinakuwa na maana fulani hasa kutoka kwa Mungu.
- B. Akawaita katika baraza lake watu mashuhuri wanajimu, wachawi, wasihiri na waganga.
1. Watu hawa waliitwa Wamakabayo, jina hilo lilitokana na watu wa kale walioishi na kutawala karibu miaka 1,000 kabla.
- C. Mfalme aliwaamuru hawa watu wenye hekima kutaja maana ya ndoto ile.
1. Kama mfalme angeweza kukumbuka ile ndoto, kwa hiyo ingekuwa ni changamoto yenye majaribu hasa kwa watu wake.
    - a) Kwa hiyo changamoto waliyopewa ni kutambua na kuelezea maana ya ile ndoto, kwa kufanya hivyo wangepewa zawadi kubwa.
    - b) Kwa kushindwa kufanya hivyo wangeonekana waongo na maisha yao kuwa hatari.
  2. Hii inaweza kusaidia kuelewa akili na jinsi alivyo Nebukadneza.
    - a) Kwa pande zote mbili Nebukadneza alikuwa katili na Mkarimu.
    - b) Pia alionekana kuwa ni mwenye akili sana kiasi cha kuweza kutambua nani alikuwa mwaminifu na nani alikuwa anamchezea (siyo mwaminifu).
    - c) Pia kwa upande wake alionekana kana kwamba anatafuta ukweli.

## III. Kuingilia kati kwa Daniel.

- A. Kwa hiyo wale watu wenye hekima waliamuriwa kuuawa baada ya kushindwa kumwambia ndoto yenyewe na tafsiri ya ile ndoto.
1. Daniel pamoja na rafiki zake walishikwa na hofu hasa kwa kuwa hawa kuwepo wakati hayo yote yalipokuwa yanafanyika hata kupewa nafasi katika swala zima la kutafsiri hiyo ndoto.
- B. Kutokana na hali hiyo Daniel aliomba muda kwa mfalme ili aweze kutafsiri ndoto yake.
1. Ukweli ni kwamba alitaka kuona uaminifu wa mfalme kwake na kutokana na ukweli kwamba mfalme alimsikia yeye (Daniel), hivyo alimpa wasaa wa kufunua na kufasiri ndoto katika hali hiyo alipendezwa na Nebukadneza.
- C. Baada ya Daniel kupewa nafasi alikwenda kukwaambia rafiki zake.
1. Wote kwa pamoja waliomba na kuomba neema na baraka kwa Mungu

kuhusiana na siri hiyo.

- a) Ni jambo la kufurahisha kuona kwamba waliomba huruma tu kwa Mungu ama msaada ungeonekana. Waliona ni vema

kungoja hadi pale Mungu atakapoweza kufunua huruma yake.

2. Mungu aliweza kumfunulia Daniel siri ya ndoto ile wakati wa usiku.
  - a) Mstari wa 18 neno “siri” katika Ki-Arabu ni “raz” ambacho ni kitangulizi katika mafunuo ya fasihi za Kiyahudi, kwa kuhusisha “Thiologia Fichika” ambayo ni mpango wa siri Mungu kuhusiana na siku ama mambo ya baadaye.
3. Daniel alimshukuru Mungu kwa kumpatia hekima na uweza pamoja na kuwajibu maombi yao baada ya kupokea ono hilo.

#### IV. Kuonekana na kufasiriwa kwa ndoto.

- A. Baada ya sala Daniel alikwenda kumuona Arioki akida aliyepewa jukumu la kuwaua wenye hekima kwa maombi ya aina mbili.
  1. Umati wote kusikia fasiri yake.
  2. Kuchelewesha kidogo kuuawa kwa wenye hekima.
- B. Nakala na masimulizi ya historia ya wafalme na falme zimekuwa ni gumzo kwa miaka mingi kuhusiana na ndoto hii.
  1. Wengi wa wasomi wanahusisha ndoto hii na matukio yanayotokea katika siku zao.
  2. Wengi wanataka kuona hii ndoto ikitimiza matakwa yao lakini sivyo.
  3. Kwa mtazamo wa ndoto hii ni mataifa ya ulimwengu katika kuimarisha

ufalme wa Mungu miongoni mwa watu.

- a) Ni kweli kwamba tawala ya kwanza katika ndoto hiyo inawakilisha Babeli (38).
  - b) Tawala ya mwisho ni ile itakayokuwepo wakati Mungu akiweka ufalme wake wa milele, ambao utabadilisha mamlaka yote ya kibinadamu.
    - 1) Ufalme ulianza kule Yerusalemu siku ya Pentekoste, Mdo. 2.
    - 2) Dola iliyokuwa na nguvu kwa muda ni Rumi.
  - c) Kutokana na habari hizi za kweli inaonyesha kuwa falme zote zingeweza kuanguka katikati ya Babeli na Rumi. Kwa hiyo maono aliyooona Nebukadneza ilikuwa ni katika kipindi cha Babeli na Rumi.
    - 1) Kichwa cha dhahabu - Wababeli.
    - 2) Kifua na Mikono ya Fedha - Tawala ya Uajemi.
    - 3) Tumbo na kiuno cha Shaba - Tawala ya Kiyunani.
    - 4) Miguu ya Chuma (Pamoja na Vidole) - Tawala ya Kirumi.
  4. Hii ndiyo tafsiri halisi ya ndoto na inabeba ujumbe wa kitabu. Moja ya fasiri yenye kuhusiana na hadithi ya Wayahudi, waliokuwa viongozi wa mwanzo.
- C. Ndoto ya Nebukadneza ina ujumbe muhimu wa aina mbili:
    1. Ujumbe uliomhusu yeye mwenyewe.
      - a) Anaweza kuwa mfalme wa wafalme (37) katika siku zake, lakini ikumbukwe kuwa ndiye Mungu wa Mbinguni aliyempa Yeye hayo.
      - b) Utawala na nguvu alizokuwa nazo zinaweza kuondolewa.
      - c) Siku zinakuja ambazo Mungu ataweka ufalme wake kati ya

watu utakaoundoa tawala za kibinadamu.

2. Ujumbe kwa ajili ya Wayahudi kule uhamishoni.
  - a) Pamoja na kuwepo utumwani chini ya tawala katili za kipagani  
bado Mungu aliongoza maisha yao.
  - b) Wakati Mungu alipoamua kukomesha falme hizi za kibinadamu,  
hivyo kuacha ufalme peke yake wa Mungu.
  - c) Kwa hiyo tena walikuwa na kila sababu ya kurudisha imani na matumaini yao pamoja na kuwa katika hali ya utumwa.

#### V. Mwitikio wa Nebukadneza.

- A. Baada ya Mfalme Nebukadneza kusikia ufunuo na fasiri kutoka kwa Daniel, mfalme alitambua kuwa hayo yametoka kwa Mungu.
  1. Baada ya hayo mfalme alianguka kifudufudi na kumsujudia Mungu na kuwa na fikra jinsi ya kumpa heshima nabii Daniel.
  2. Nebukadneza akamweka Daniel kuwa mkuu zaidi ya maliwali wote.
- B. Mwitikio wa Daniel ulikuwa wa unyenyekevu na upole.
  1. Aliweza kukumbuka maombi yaliyofanywa pamoja na rafiki zake hivyo akaona ni vema nao kupatiwa nyazifa.
  2. Alionyesha shukrani, kwa kufanya hivyo ilikuwa ni msaada kwake kwa siku za baadaye kwa kutambua kuwa wapo watu waaminifu kwenye nyumba yake.

### Daniel, Sura 3.

#### Sanamu ya Dhahabu na Tanuru la Moto Mkali.

#### I. Sanamu ya dhahabu ya Nebukadneza.

- A. Kipindi cha matukio haya hakijulikani sawasawa.
  1. Matukio haya yalitokea baadaye kuliko yale yaliyotokea katika sura ya  
2.  
a) Mistari 12-30 ni kabla ya Shadraki, Meshaki na Abednego kusimikwa.
  2. Sanamu katika sura ya 2 pengine ni kitangulizi cha ile aliyojenga katika sura ya 3.
  3. Wakati huu Daniel hakuhusika.
- B. Chanzo na lengo la sanamu hii haliko wazi.
  1. Habari haielezei kwa undani zaidi hii sanamu ilikuwa inawakilisha kitu gani.
    - a) Je, tawala ya Babeli?
    - b) Pengine Nebukadneza.
    - c) Pengine Bel, Mkuu wa Babeli.
  2. Inawezekana mawazo yote haya yalilengwa kuhusiana na sanamu yenyewe.
    - a) Katika siku hizo, watawala, mfalme na Mungu zilikuwa zinaonekana kama kitu kimoja.
    - b) Pengine kuanguka kifudufudi mbele ya sanamu kama ilivyo hapa, ingekuwa ni moja ya kutambua na kutoa heshima kuu kwa



vyote vitabu.

C. Kwa wapagani, watu wasio na dini mateso na unyanyasaji ulidhamiriwa kwa

kuanguka kifudufudi kama heshima kwa miungu yao.

1. Hakukuwa na sheria kinyume na kuabudu miungu wengine isipokuwa

Nebukadneza hapo alitaka kuongezea nyingine zaidi kati ya zile

zilizokuwepo.

2. Yote hayo ilikuwa ni kutaka kutambulisha kuwa mfalme wa Babeli na

miungu yao walikuwa ndio wakuu kuliko wengine.

a) Inawezekana tangazo hilo lilikuwa ni la kisiasa zaidi kuliko

kidini.

b) Kuiga imani za kipagani kwa siku zile lilikuwa jambo la

kawaida hasa ukizingatia kuwa mfalme alionekana kama Mungu.

3. Mataifa yote chini ya Babeli katika siku zile isipokuwa Wayahudi walipata shida ya kusujudia ile sanamu.

a) Hakuna mfalme katika siku zile aliyeamini kuwepo kwa Mungu mwingine zaidi yake kwa kuwa waliamini kuwa wao ndio

Mungu.

b) Kwa hiyo kutokana na uzoefu wao, kwa yeyote ambaye

hakufuata mpango wao wa kuabudu alionekana kuwa ni muasi na haini.

## II. Shutuma dhidi ya Shadraki, Meshaki na Abednegi.

A. Wakati jambo la kusujudia sanamu lilipowekwa, mikoani mwa

“Wamakabayo”(Wenye hekima wa Babeli katika siku hizo), waliwashutumu vijana watatu wa kiyahudi kwa kutofuata amri ya mfalme.

1. Walishutumiwa kwa kutosujudia miungu ya Babeli na kwa kutokuwa

waminifu kwa mfalme.

B. Wakati Nebukadneza aliposikia kwamba kuna watu wasiotaka kusujudia sanamu alighadhabika sana, akatulia kidogo kabla ya watu wale kuwekwa mbele yake.

1. Pengine ni kutokana na uaminifu waliokuwa nao hao vijana kwa siku

zilizopita, kwa hiyo aliamua kuwapatia nafasi nyingine kwa kufikiria

kuwa pengine hawakuelewa hapo kabla.

2. Katika kufanya hivyo, anawaelezea tatizo lao la kukataa kusujudia sanamu.

a) Akiwaonya kuwa wakishindwa kufanya hivyo, “Mungu gani atawaokoa kutoka mikono ni mwangu” (mstari 15).

C. Jibu la Shadraki, Meshaki na Abednego.

1. Walikuwa tayari kuelezea sababu mbele yao bila kujali kitu chochote.

2. Walijibu kirahisi na kukiri kuwa Mungu wao ni mwenye nguvu zote na

yeye atawaokoa kutoka mikononi mwa mfalme.

- a) Kwa hiyo hawakuwa tayari kuinama na kusujudia na kuabudu sanamu.

### III. Tanuru kali.

- A. Walijibu kwa namna ile iliyomuudhi mfalme.
1. Kwanza walimwita mfalme kwa jina wakati wafalme katika siku zile ilikuwa siyo rahisi kuitwa majina yao.
  2. Pia nafsi yake iliumia kuona watumwa waliokuwa wanatumika mbele yake, sasa hawapo tayari kutii amri ya mfalme.
- B. Kwa hiyo aliamuru tanuru kuwekwa moto zaidi ya ilivyokuwa kawaida yake.
1. Pengine waliweka mafuta kwenye mlango ili moto uwake zaidi kama wa kuokea ama kuchomea au kuunguzia vitu.
  2. Watu hawa waliwekwa hali wamevaa nguo huku mfalme akikaa mkao wa kuangalia mambo jinsi yalivyokuwa yanaendelea.
    - a) Mambo yalianza kulipuka wakati walenzi wa Nebukadneza walipungua katika harakati za kuwatupa hawa ndugu ndani ya tanuru.
    - b) Mfalme aliona sura ya nne ndani ya tanuru na sura zote hizo hazikuzulika, zilionekana kama wana wa miungu.
    - c) Tafsiri zingine, “Kama mwana wa Mungu” lakini tafsiri nzuri ni hiyo inayopatikana katika kifungu “b.”
    - d) Baadaye akatambua kuwa katiya wale (28) mmoja wao alikuwa ni malaika.
- C. Baada ya kuona kwamba hawa watu walikukwa salama, akaamua kuwaita nje ya tanuru.
1. Baada ya kutambua kuwa walikuwa watumishi wa Mungu aketiye mahali pa juu.
    - a) Kwa njia hiyo alikiri kuwa Mungu wao ni mkuu kuliko vyote.
    - b) Lakini bado hakutambua kuwa Mungu wa Israel ni mmoja na Mungu pekee hakuna Mungu mwingine.
    - c) Kwa njia hiyo alijifunza (alikiri) kwamba ile sanamu kubwa siyo kitu mbele ya Mungu.

### IV. Matokeo tokana na tukio hilo:

- A. Kipindi kati ya ufasiri wa ndoto na tukio hili hakijulikana.
1. Inaonyesha kwamba mambo yote mazuri yaliyotendeka kwa kupitia Daniel, kwake yeye hayo alikuwa ameshasahau na ndiyo maana hapa anashangaa tena.
- B. Pamoja na Nebukadneza kutambua kuwa Mungu wa Daniel ni mkuu kuliko vyote lakini bado hakufahamu kuwa Mungu huyo ni Mungu peke yake.
- C. Kutokana na tukio hili alihalalisha ibada kwa Mungu na kwa yeyote ambaye angeonekana kupinga angepata matatizo.
1. “Kwa kuwa hakuna Mungu mwingine anayeweza kuokoa namna hii!”
- D. Baada ya hapo, matumaini ya wale wote walitaka kuwaharibu hawa ndugu yalipotea pale mfalme alipowatawadha na kuwaweka mahali pazuri kuliko mwanzo.

---

## Sura 4

### Njozi ya Mti ya Nebukadneza

#### I. Barua ya Nebukadneza

- A. Barua iliandikwa kwa nia ya kusomwa kwa wote waliokuwa chini ya miliki yake.

1. Aina hii ya Uandishi kwa kawaida ulitumika katika kuchapa

sheria mpya, kuweka sheria mpya, katika maswala ya kodi n.k..

2. Katika barua hii mfalme anakiri ukuu wa Mungu wa kigeni pamoja na mtawala wake.

B. Mtindo wa Uandishi katika sura hii.

1. Mistali 1- 18, kukiri kwa uwazi, njozi imeandikwa katika hali ya nafasi ya kwanza.
2. Mistali 19 -33, fasiri na utimilifu wa njozi umeandikwa katika hali ya nafasi ya tatu.
3. Mistali ya 34 -37, ikielezea kudhurika na kuchafuka kwa Nebukadneza pamoja na hitimisho la kukiri kwake yameandikwa katika hali ya nafasi ya kwanza.

**II. Ndoto.**

A. Muda haujulikani kuhusiana na matukio haya:

1. Pengine habari hii ilikuwa ni mwishoni mwa utawala wake, kutokana na vitu vyake vya ushindi (605 - 562) na kujenga miliki yake vilikuwa vimefikia kikomo.
2. Matunda ya kazi yake yalimfanya kuwa na kiburi, mwenye kujiamini na mbinafsi.
3. Lakini majivuno yake yaliharibiwa na ndoto.

B. Akaanza tena kutafuta tafsiri ya ndoto hiyo kama alivyofanya katika sura ya 2.

1. Kwa ujumla njozi ile ilikuwa na mambo mengi haikuzingatia kiini/eneo fulani tu.
2. Ndoto iliharibu umaarufu wa Wakadayo waliokuwa nao.
3. Daniel alionekana kama mtu maarufu hasa katika mambo yale yasiyo ya kawaida.
  - a) Kwa hiyo alitafutwa na mfalme. Kama yeye mhusika na “Roho za Miungu”.
4. Daniel hakumweleza mfalme Nebukadneza maana yake pengine tu mambo yaliyohusiana na utawala wake na jinsi alivyomtendea mema.
  - a) Lakini mfalme alitaka aambiwe ukweli.

C. Sura au mwonekano wa njozi hii kiasilia inajidhihirisha, na haikuwa kawaida kwa Mungu kuzungumza na watu kwa njia hiyo.

1. Mti.

- a) Alama ya uzima ukiwa na enzi za kifalme na mwendelezo wa ufalme.
- b) Kwa kupambanua mti kwa maneno ya “Kiaramaiki” na “Uungu” karibu yanaelezea kitu kilekile, “Iylan” inamaanisha mti wakati “elah” inamaanisha “Miungu”.
- c) Ukuaji sana wa mti unahusisha maono katika hali ya kupokea utakatifu / utukufu.
- d) Matawi yanasimamia tawala za kisiasa ulimwenguni.
- e) Matunda na majani yanasimamia utajiri na fahari.
- f) Kwa hiyo viumbe vyote vinategemea mti kwa kila kitu.

2. Hukumu ya Mti.

- a) Tangazo kutoka kwa yule mjumbe inaonyesha kwamba hukumu imetoka kwa Mungu.
- b) “Ukateni hata nchi” uliaminiwa kuwa wenye utukufu na sasa hali imegeuka.
- c) “Punguza matawi yake, yapukutisheni majani yake na kuyatawanya matunda yake,” ni kuondolewa nguvu zake za siyasa na utajiri.
- d) “Na wanyama wakimbie,” kupotea kwa utawala wake kwa watu.

3. Ukuaji tena wa Mti.

- a) Kisiki na shina yalifungwa kwa chuma na shaba ambayo yaliwekwa wazi. Mstari huu ni Ki-Arabu ambao unasomeka kama “Mizizi”.
- b) Hapa ni wazi kwamba ono hili lilikuwa linamuhusu mtu.
  - 1) Mtu ataloweke kwenye umande na kuishi kama mnyama.
  - 2) Kwa kupoteza uwezo wake wa kufikiri, mtu ataonekana kama mnyama.
- c) Hali hii itaendelea kwa “Vipindi saba.”
  1. “Iddan” (Ki-Arabu) inaonyesha kuimarika kwa au kuishi kwa kipindi kilichokuwa kinajulikana au kutojulikana. (Nyakati)
  2. Vipindi saba wasomi wengi wanatofautiana:
    - a) Siku saba.

- b) Majira saba.
- c) Muda kamili uliowekwa na Mungu.

### III. Tafsiri ya ile ndoto.

- A. Kama zile ishara zimeeleweka ni wazi kwamba ndoto inajifasiri yenyewe.
  - 1. Yote ni kwa ajili ya mtu.
  - 2. Utatuzi wake ni pale Daniel alipomweleza mfalme kwamba yeye ni mtu.
- B. Pamoja na ukweli kwamba ndoto ile ilikuwa ni onyo, mfalme angeweza kutubu hakuna kitu kibaya ambacho kingetokea, Eze. 3:17-21.

### IV. Utimilifu wa ile ndoto.

- A. Mwitikio jirani kuhusu ile ndoto haujahifadhiwa.
  - 1. Alichukulia umakini maneno ya Daniel kwa kitambo kifupi, tangu hapo  
 ikapita mwaka kufikia utimilifu wa ile njozi.
  - 2. Mwishoni mwa mwaka utukufu wake ulishusha na kufedheheka kiasi  
 cha maisha yake kubadilika ghafla.
- B. Uthibitisho zaidi kuhusu kudhurika na kuchafuka kwa hali ya mfalme ni adimu.
  - 1. Mmoja wa watu aliyetwa Berosus, mwana historia wa Kibabeli aliwahi  
 kuandika kwamba mfalme alitangulia kuugua kwa muda kabla ya  
 kufariki hii ilikukwa yapata miaka 250 baada ya Daniel.
  - 2. Mwana historia mwingine aliyetwa Abydenus aliandika katika karne ya pili (2) B.K.,  
 kutokana na kumbukumbu za Kibabeli kwamba, inasadikika  
 baada ya Nebukadneza  
 kushindwa alipanda juu ya mnara wa kifalme na alichukuliwa na “Mungu fulani”.
    - a) Hivyo akatangaza kuwa tawala ile ingeweza kuangukia kwa utawala wa  
 Uajemi ukiunganika na Umedi pamoja na Miungu ya Babeli.
    - b) Aliomba kwa ajili ya maangamizi ya Waajemi.
    - c) Aliomba kufa kifo kizuri.
    - d) Kufuatana na masimulizi aliondolewa katika wadhifa wake.
    - e) Masimulizi haya yanafanana na Daniel sura ya 4
  - 3. Maelezo haya yalipatikana kutokana na kipindi cha Nebukadneza.

*“Kwa muda wa miaka minne kiti cha ufalme wangu katika mji wangu.....haukufurahisha moyo wangu. Katika miliki yangu yote sikujenga na mahali pa juu, hazina katika ufalme wangu sikuweka wazi. Katika ibada ya Bwana wangu Merodak, furaha ya moyo wangu katika Babeli, mji wa milki yangu, wala sikumtukua kwa nyimbo, wala kulisha madhabahu yake, wala kusafisha mifireji.”*

- C. Kwa mtazamo wa nje aliokuwa nao ndio huo waganga wanaoitwa “Boanthropy”.
  - 1. Huu ni ugonjwa wa akili inapotokea mtu kufikiria kana kwamba yeye ni ng’ombe .
  - 2. Mambo kama haya siku za leo siyo mara kwa mara kutokea, lakini yanafahamika.

### V. Mfalme aliyebadilika.

- A. Baada ya “nyakati saba” kupita, Nebukadneza alirudiwa na afya yake ya awali.
  - 1. “Nikainua macho yangu kuelekea Mbinguni”. Msemo wa Kiswahili kwa maana  
 kwamba, anafahamu na kutambua kwamba utawala wake ni kwa mapenzi ya Mungu.
  - 2. Ukilinganisha mistali ya 34b na 3b inaonekana kama zaburi.
- B. Baada ya kurudiwa na akili yake, alirudia na kuchukua wadhifa aliokuwa nao kabla kutoka kwa Mtawala aliyekuwa anatawala.
  - 1. Anaonekana tofauti kabisa, kuhusu yeye mwenyewe, na Mungu wa  
 Daniel aliyemwita Mungu aliye juu.
    - a) 2:11, “Mungu ...haishii miongoni mwa watu.”
    - b) 4:35, Naye hufanya kama atakavyo katika jeshi la Mbinguni na  
 katika hao wanaokaa duniani.

2. Mamlaka yake hayakuondolewa, lakini alitambua ukweli kwamba yeye ni mwanadamu.
- C. Hapa ikawa ndio mwisho wa historia katika Biblia kuhusu Nebukadneza.

#### VI. Masomo tuliyojifunza katika sura ya 4.

- A. Tusijivunie vitu tulivyonavyo, Lk. 12:20.
- B. Yehova anachukia moyo wenye majivuno, Rum. 12:3; 1 Kor. 11:28.
- C. Watu walioshawishiwa na nguvu za Mungu wanatafuta ukweli, Mat. 28:18; 2 Tim. 4:2.
- D. Wakati fulani hali ngumu zaweza kubadilika na kuwa maisha ya furaha ukijiweka karibu zaidi na Mungu.
- E. Tunaweza kuwa watu wa Mungu kwa kuwa waaminifu, 4:1-3.

### Daniel 5

#### Maandishi Ukutani

#### I. Kutoka Nebukadneza mpaka Belshaza.

- A. Baada ya Nebukadneza kuona ukweli kuhusu Mungu akawa mfuasi wa taratibu za Kiyahudi. Hii ikapelekea kuwepo kwa mtengano katika familia.
- B. Nebukadneza alitawala kwa muda wa miaka 43.
  1. Alifuatwa na Evil-Merodaki aliyetawala kwa muda wa miaka miwili.
    - a) Alijulikana kwa wema wake kwa mfalme Yehoyakimu aliyekuwa amefungwa kwa muda wa miaka 37 chini ya Nebukadneza.
    - b) Aliuawa na shemeji yake baada ya miaka miwili pengine kutokana na imani yake kwa dini Kiyahudi.
  2. Nergal-Sharezer alitawala kwa muda wa miaka sita baada ya kuuawa kwa Evil-Merodaki.
  3. Baadaye alikuja kutawala Nergal kwa muda wa miezi 9 na akauawa na wafuasi wake.
  4. Mmoja kati ya wafuasi wake aliyeitwa Nabonidus alitawala kwa muda wa miaka 17, na akawa mtawala wa Babeli ilipoangukia kwa tawala za Umedi-Uajemi.
    - a) Alikuwa ni mtu aliyezoolea mambo ya uganga na uchawi na alimkana Mungu pamoja na kuwadhihaki viongozi waliomwamini Mungu.
    - b) Muda mwingi alibaki Tema wala hakutembelea Babeli.
    - c) Mwana wa Belshaza alitawala kama kaimu ndiye aliyeleta uthibiti katika taifa.
      - 1) Baadhi ya kumbukumbu rasmi zinaonyesha kuwa baba yake alikuwa mfalme lakini maamuzi yalikuwa kwa mtoto wake.

#### II. Karamu ya Belshaza.

- A. Katika sura ya tano inaonyesha jinsi Babeli ilivyoangukia mikono mwa waajemi.
  1. Ukiangalia jambo hili, utaona kweli Babeli ilikuwa katika hali ya kuanguka, taifa lilikuwa likishambuliwa lakini viongozi wao walikuwa wakisherehekea mamlaka yao.
  2. Alikuwa akisherehekea pamoja na wafuasi wake kwa miungu yao ambayo Baba zao waliona siyo kitu.
  3. Pengine aliweka mpango huu ili kuweka imani kwa watu wake ambao walianza kutokuwa na moyo na serikali yake, kwa hiyo aliona pengine hii ndiyo njia ya kurudisha imani kwake.
- B. Katika hali ya kusherehekea sikukuu aliomba kurudishwa kwa vyombo vilivyochukuliwa kwenye hekalu la Mungu, na watu kuanza kuvitumia kwa kunywea.
  1. Kwa kufanya hivyo alionyesha dharau na matusi kwa imani ya Kiyahudi na wale watu waliomfuata Yehova kwa kumheshimu Marduk akitumia vyombo kutoka Yerusalemu. Pia kwa kufanya hivyo akawa anamkumbuka yule shujaa wa Babeli Nebukadneza.

2. Nadharia zinapatikana hapa ni kwamba, alikuwa akimkufuru Mungu katika ibada hiyo ya kipagani kwa kutoa matusi.

### III. Maandishi Ukutani.

- A. Walevi walibadilika baada ya kuona mkono bila kujua ulikotokea na kuandika ukutani katika karamu ya mvinyo.
  1. Maandishi haya hayakueleweka kwa Belshaza hata kwa wageni wake.
  2. Pengine Mtindo wa Uandishi haukuwa tofauti kutokana na kwamba hakukuwepo na Irabu, kwa hiyo ilikuwa ngumu kwao kuelewa bila ya mtafsiri.
  3. Katika hali ile ile mfalme aliamua kutia mali na zawadi kwa yeyote ambaye angeweza kusimama na kufasiri maneno hayo.
    - a) Kwa mtu ambaye angeweza kufasiri aliahidiwa kuwa mtu wa tatu katika ufalme, baada ya yeye mfalme na mwanaye mfalme Belshaza.
    - b) Kama kawaida tena waliitwa Wamakabayo na wakashindwa.
- B. Hapa tunatambua kwamba Belshaza hakumjua Daniel hata kidogo.
  1. Daniel inawezekana pengine alikuwa nje kwa huduma za serikali.
  2. Kwa wakati huu Daniel alikuwa na umri kama wa miaka 80 hivi.
  3. Pengine kwa wakati huu Daniel alikuwa ameshushwa katika wadhifa wake kutokana na mabadiliko ya uongozi.
  4. Hivyo malkia anamkumbusha mfalme Belshaza kuhusu Daniel.
 

Aliyemtumikia Nebukadneza vizuri.

    - a) Pengine malkia alikuwa mshenga wa Nabonidus.
    - b) Wake zake walikuwa katika karamu ya divai isipokuwa malikia aliingia baada ya kusikia tukio hili.
    - c) Tangu Nabonidus kuwa mfalme hasa, mke wake akawa na heshma ya umalkia.
    - d) Kutokana na uzee wa mama yake Belshaza, hata hakuweza kukumbuka matendo makuu aliyofanya Danieli.
- C. Kutokana na kusihi kwa mama yake Belshaza, alimwita Danieli.
  1. Kwanza Danieli hakuwa na haja ya vitu ama zawadi, yeye aliamua kusima na kufasiri yale maneno.
  2. Kabla ya kuwaeleza maana ya maneno hayo Danieli aliwahubiria kwanza.
    - a) Danieli aliwakumbusha uwezo na nguvu za mungu zilizoonekana katika enzi za Nebukadneza.
    - b) Kwamba nguvu za Yehova ni ushuhuda kamili na kuwa ni swala la kukumbukwa. Kwa hiyo mfalme amemdharau Mungu mwenye kutawala miliki zote.
    - c) Kwa hiyo majaaliwa yake yamefikia kikomo na kufunuliwa kwa njia ya maandishi ukutani.

### IV. Tafsiri ya Maandishi.

- A. Daniel alisoma yale maelezo kwa maneno manne: MENE, MENE, TEKELI na PERESI.
  1. Kifungu hiki cha maneno kinaonekana kana kwamba ni katika hali ya uthamanishaji wa bidhaa za biashara na kipimo cha Fedha cha Dola.
  2. Lakini maneno haya kama yalivyo maneno ya kiingereza “Pounds” na “halves” yanaweza kutumika kama majina au vitenzi, yakiwa na maana yenye kutofautiana yakitegemea kama ni jina au tendo.
- B. MNH “Mene”
  1. Kama jina ina maana ya shekeli 60.

2. Kama tendo lina maana ya “kupima”, au “kuhesabu”.
  3. Kwa kuwa neno MENE limetajwa mara mbili, inaonyesha kwamba moja  
ni tendo na lingine jina.
  4. “Ikihesabika katika mizani.”
- C. TKL “Tekel”
1. Kama jina ni Shekeli.
  2. Kama tendo ina maana ya “Kupungukiwa”.
- D. PRS “Peres”
1. Jina kwa maana ya “nusu”.
  2. Kama tendo lina maana ya “Kugawanyika sehemu sehemu/vipande”.
  3. Konsonanti zenye kupatana lakini zenye maana tofauti zinatamkwa kama, Ujemi!
- E. Hapa ni rahisi kuona kwamba hakuna mtu aliyeweza kuelewa isipokuwa mwana wa Mungu.
1. Fasiri ya Daniel ikufunua maana zaidi ya “Kupima katika mizani, shekeli na nusu nusu.”
    - a) MNH - Maana yake ni kwamba maisha ya Belshaza yamepimwa na kuchunguzwa na Mungu.
    - b) TKL - Inaonyesha kwamba Belshaza ameshindwa.
    - c) PRS - Inaashiria kwamba ufalme wake umegawanywa kwa Wamedi na Waajemi.

#### V. Kuanguka kwa Babeli.

- A. Pamoja na Daniel kukataa thawabu kutoka kwa mfalme lakini anaonekana mwenye vitu vingi.
  1. Maana ya “wa tatu katika ufalme” hakikuwa kitu kikubwa katika ufalme, hakungoja kesho yake.
  2. Usiku ule ule Kureshi aliteka Babeli na kuingia mjini pasipo upinzani na Belshaza aliuawa.
- B. Kwa hiyo ufalme ukachukuliwa na Dario kutoka Medi.
  1. Kutokana na nakala zinaonyesha kwamba Kureshi kuktoka Uajemi alipiga Babeli, hii ilitabiliwa na Isaya katika 44:28; 45:1,13.
  2. Mji wa Babeli ukafanywa jimbo.
  3. Pengine Dario alikuwa ni kibaraka wa Kureshi kama vile Herode alivyokuwa chini ya Rumi.
- C. Dario alikuwa na umri wa miaka 62 alipochukua madaraka.
  1. Sababu ya kuhesabu/kumbukumbu ya umri pengine ni kutokana na “60 + shekeli (61) + nusu mbili = 62”!

#### VI. Utawala wa Babeli ulikomeshwa baada ya miaka 86.

### DANIELI 6

#### Danieli Katika Shimo La Simba

#### I. Dario alimweka Danieli katika nafasi yenye mamlaka, 1-3

- A. Dario aliweka maliwali 120 katika utawala wake.
  1. Liwali ni mtawala aliyekuwa na mamlaka katika uongozi wa wananchi  
na jeshi na aliongoza jimbo lote.
- B. Dario alichagua rahisi watatu juu ya hao maliwali.
  1. KJV inaeleza kuwa Danieli alikuwa juu ya wote lakini maelezo hayo si  
sahihi kwani wote walikuwa sawa katika mamlaka.
- C. Lakini Danieli kwa kutembea na Mungu alionyesha tofauti yake juu ya hao marahisi na maliwali
  1. Roho bora alikuwa juu yake.

## II. Wivu na kijicho vinasababisha kufanya shauri la kumwondoa Danieli 4-9.

- A. Mstari wa 4-5 marahisi pamoja na maliwali wanatafuta sababu ya kumchongea kwa mfalme.
1. Kwanza walijaribu kutafuta makosa juu ya kazi yake ili aondolewe kwenye nafasi yake.
  2. Wengine walikuwa wanatumia nafasi zao kwa manufaa yao.
  3. Lakini hawakuweza kupata kosa katika kazi ya Danieli.
- B. Baada ya kushindwa wanaamua kutumia imani ya Danieli dhidi yake.
1. Wakamsihi mfalme aweke sheria ya kuzuia mtu yeyote asimwombe Mungu mwingine, ama mtu mwingine kwa siku 30, Yoh. 8:44; 2 Kor. 11:3; Mith. 14:30.
  2. Walijua Danieli amejitoa kwa Mungu na hivyo angechagua Mungu badala ya binadamu.
- C. Hivyo wakamwomba Mfalme kuweka sahihi kwenye hayo maandiko.
1. Walijua kwamba baada ya kuweka kiapo chini ya sheria kama wafanyavyo Waamedi na Waajemi basi haitatenguliwa, Est. 1:19, 8:8.

## III. Maombi ya kijasiri ya Danieli dhidi ya madai ya washitala wake 10-15.

- A. Danieli aliendelea kumwomba Mungu mara tatu kwa siku akiwa amefungua madirisha.
1. Maombi kwa Yerusalem ambayo ilikuwa mila ya zamani, 1 Fal. 8:33, 35, 38, 44, 48; Zab. 5:8; 28:2.
- B. Mstari wa 11-12 tunaona kuwa maadui wa Danieli walikuwa wanasubiri Danieli avunje tamko hilo.
1. Walimwomba akiomba wakaenda kutoa ushahidi kwa mfalme
    - a) Walimwita "...Mmoja wa watoto wa watumwa wa Yuda..."
    - b) Danieli alikuwa mtu mzuri aliyemweshimu Mungu kuliko mfalme, Mdo. 4:19-20, 5:29.
- C. Majibu matatu ya Dario.
1. Hakufurahi kwa kuwa alikuwa anathamini kazi ya Danieli.
  2. Hakufurahi kwa kuwa alielewa kuwa wamemdanganya.
  3. Alitafuta njia ya kubadirisha sheria ama adhabu usiku nzima.
    - a) Kujaribu kumbadilisha Danieli imani yake.
    - b) Lakini viongozi kwa ubinafsi wao wakamkumbusha Mfalme juu ya sheria ya Wamedi na Waajemi msitari wa 15.

## IV. Amri ya kusita ya Dario, 16-18.

- A. Mfalme anaonyesha kuwa Mungu angemwokoia Danieli
1. Haikuwa usemi wa imani ila ni msemu tu uliokuwa unatumiwa na wote waliokuwa wanaamini kwamba mungu yeyote aweza kuokoa imani zao.
  2. Ulikuwa usemi mzuri kwa Danieli.
- B. Pango la simba ilikuwa ni aina ya mauaji ama adhabu kwa siku zile.
1. Walikuwa wanazungusha jiwe juu ya shimo kuzuia watu wasiweze kuwaokoa.
  2. Kwa kawaida Mfalme au Mtawala alikuwa anaweka mhuri yake.
- C. Ndipo wakamweka Danieli kwenye shimo kisha Mfalme akarudi nyumbani kwake.
- D. Dario anaonyesha masikitiko yake kwa yaliyotokea katika njia tatu.
1. Alikesha usiku kucha.
  2. Vinanda havikuletwa kwake.
  3. Hakuweza kupata usingizi.

## V. Mungu anamwokoia Mtumishi wake Danieli 19-23.

- A. Angalia wasiwasi kwenye uso wa mfalme kwa matendo yake asubuhi iliyofuata.
1. Aliamuka mapema na kwenda kwenye shimo.
  2. Akamwita Danieli kwa sauti ya kubembeleza



- B. Katika mstari wa 21-22 baada ya Danieli kumsabahi Mfalme, akamweleza kuwa Mungu amefunga vinywa vya simba.
1. Kwa kuwa hakuwa na hatia mbele za Mungu, hakufanya dhambi, alionewa kwa kufanya mapenzi ya Mungu.
  2. Pia Mungu alimwacha kwa kuwa hakufanya lolote baya kwa Dario.
  3. Mstari wa 23 tunaona kuwa aliokolewa kwa kuwa alimwamini Mungu,

Mit. 3:5-6 Gal. 5:6; Yak. 2:14-26.

## VI. Jinsi Mfalme alivyopokea Ukombozi wa Mungu kwa Danieli 24-28.

- A. Washitaki wa Danieli wote wakatupwa kwenye shimo la simba pamoja na wake zao na watoto wao, Gal. 6:7-8; Hos. 8:7; Mit. 11:8.
1. Simba walikuwa na njaa sana na wakali kiasi kwamba wale watu waliuawa hapo hapo.
  2. "Kushitaki" katika lugha yao ina maana, "...kula vipande vya mtu."
  3. Yote hii ilikuwa haki kwa taratibu za mashariki.
- B. Tamko la Dario ni sawa na la Nebukadneza, 3:28-29.
1. Kwamba mtu ni lazima aogope na kutetemeka mbele za Mungu aliye hai.
  2. Pia anamweleza Mungu kama mshindi na mtawala kwa milele na ufalme
- wake utakaa milele, 2:44; 4:2-3.

## Danieli 7

### Ndoto ya Danieli Kuhusu Wanyama Wanne

#### I. Utangulizi:

- A. Hii sura inaanza mabadiliko kubwa ya kitabu hiki.
1. Sura 1-6, Nyalaka za matukio ambapo nguvu za Mungu na utawala wake duniani unaonyeshwa katika viongozi wapagani kwa Yuda walipokuwa utumwani Babeli.
  2. Sura ya 7-12 inahusu maono ya nguvu aliyoyapokea Danieli kuhusu maisha ya baadae ya Waebrania na kuanguka kwa milki ya Babeli.
- B. Sura ya 7-12 ina muda wa utaratibu wake.
1. Matukio katika sura sita za kwanza zimetumia kipindi cha miaka 67, 606 - 539.
  2. Maono katika sura ya 7-12 yamefunuliwa nyakati tofauti kati ya 549 na 536.
- C. Maono manne katika 7-12, sura tatu za kwanza (sura 7,8, & 9) ni utabiri.
1. Neno "apocalyptic" linatokana na neno la Kiyunani "apokalyptein" lenye maana ya 'kufungua; au kufunua jina la kitabu cha ufunuo katika Kiyunani ni Apokalupsis.
  2. Maono ni kazi ya fasihi ambayo inaonyesha jinsi ambavyo Mungu anajibu ambapo anaangamiza nguvu zinazotawala za uovu na kubadilisha kwa haki.
  3. Tabia ya maono ina maana ya:
    - a) Tarakimu za kialama/ishara - muunganiko wa namba fulani zikiwa na eleza sifa za Mungu, mwanadamu au talatibu za mambo ya asili.
    - b) Sanaa ya maandishi: ni ya kuvumisha hata kubuni maneno picha yametumika kuvutia na kusisitiza umuhimu na thamani ya misingi ya kanuni zake.

#### II. Wanyama manne.

- A. Labda kuwepo maelezo ya kutosheleza vinginevyo (mstari I) sura ya ufunguzi imeandikwa kwa
- mtu wa kwanza.
1. Inaonekana kuwa ni - Mwandiko wa Danieli mwenyewe.
  2. Ukweli kwamba sura ya 7 imeandikwa kwa kiaramaik haina maana yoyote, Wayahudi walipokuwa utumwani walijifunza hiyo lugha na lugha za makabila yao zilikosa nguvu.
    - a) Pia hii sura yaweza kuwa ilichukuliwa maandishi ya Danieli mwenyewe.
  3. Sura ya 8-12 iliandikwa na nafsi wa kwanza na Danieli lakini kwa lugha yake ya

Ki-ebraia, sura hizi zaweza kuwa zilichukuliwa toka kwenye majarida ya binafsi ya Danieli.

B. Katika ndoto yake, Danieli aliona pepo nne za mbinguni zikisukuma bahari kuu ulikosababisha wanyama wakubwa wanne wasimame.

1. Bahari kubwa yaweza kuwakilisha uwingi wa watu wajazayo nchi, Ufu. 17:1, 15; Isa. 17:12-13; 57:20.
2. Pepo nne zaweza kuwa zinawakilisha nguvu zisizoonekana na kazi ya Mungu katika historia ya binadamu.
3. Wanyama wanne ni mfano wa utawala wa duniani, ambao ingawa ulikuwa walitiwa nguvu na Mungu, hawakutoa shukurani bali walionyesha uhasama kwa Mungu na waminifu wake.

C. Kwa kusaidiwa na historia ni raisi kwetu kuwatambua hao wanyama wanne katika ndoto ya Danieli.

1. Wa kwanza ni Babeli.
  - a) Sifa ya simba inaonyesha utukufu na uwezo wa waliokuwa nayo katika milki ya Nebukadneza.
  - b) Maangamizo ya milki hii ya kudhalilisha kwa kuwa walishindwa hata bila ya kupigana.
2. Mnyama wa pili, anawakilisha milki ya Wamedi na Waajemi.
  - a) Kama dubu, ilikuwa taratibu lakini yenye nguvu na hamu ya kumeza adui yake.
  - b) Mwinuku kwa upande moja wa mnyama yaweza kuwa ni kidokezo cha utawala wa Wamedi na Waajemi, na inaonyesha jinsi Wajemi watazidi nguvu kuliko Wamedi.
  - c) Mbavu tatu mdomoni mwa mnyama yaweza kuwa mfano wa ushindi kubwa ambaye anameza kila kitu, lakini yaweza pia kuwakilisha milki tatu za awali ambapo Wajemi ilizimeza Babeli, Misri na Lydia.
  - d) Amri ya “inuka na ule nyama mpaka utashiba!” Inaonyesha ukweli kuwa hii milki ilitegemea kupata nguvu yake na mamlaka yake kwa mamlaka kubwa zaidi.
3. Mnyama wa tatu anawakilisha milki ya Hellenistic ya Alexander Mkuu (III) ya Makedonia na warithi wake.
  - a) Kuwa kinyume ya Dubu ya Waajemi, mfano wa chui lenye mbavu nne inaonyesha kasi ya ajabu ambayo Alexander alichukua ufalme wake toka kwa Aegeni mpaka mipaka ya magharibi ya India, kabla hajafa mwaka 33.
  - b) Vichwa vinne yaweza kuwa mambo manne ya Alexander.
    1. Ptolemy
    2. Seleucis
    3. Lysimachus
    4. Cassander
  - c) Ambaye aligawanya ufalme wa Alexander katika majimbo manne.
    1. Misri
    2. Ushuru - Mesopotamia
    3. Asia ndogo
    4. Uynani
  - d) Tena mnyama wenye mabawa manne alipewa nguvu zake toka juu na majimbo manne yasingetokea bila mawimbi manne ya mbinungi.
4. Mnyama wa nne anasimamia Utawala wa Rumi.
  - a) Ni ufalme wa kutisha na hakuna mnyama inaweza kusimama kwa niaba yake.
  - b) Tunaone mnyama huyu ni tofauti kwa kuwa ana mapembe kumi.
    - 1) Wakati Danieli anachunguza mapembe kumi ya kumi na moja yalitokea.
    - 2) Na pembe huyu ananyoa mapembe tatu ya kwanza.
    - 3) Pembe ndogo anamacho ya mwanadamu (maana yake yeye ni mwanadamu, na maonyo yake siyo mazuri, na hekima finyo na

anaelewa kidogo.

a. Lakini mdomo wake ni ya kujivuna (anajivuna uungu wake?)

4) Matendo ya pembe ndogo inatafutisha yeye kati ya mapembe mengine (au wafalme wengine).

## II. Hukuma ya Mnyama wa Nne.

- A. Wakati Danieli anaendelea kutazama mnyama wa nne na kushagaa kuhusu matendo yake, tunaona habari inabadirika kutoka ulimwengu huu kuingia mbinguni; tena maandishi ya hapa yalikuwa nathari lakini saa hizi maandishi yanabadilika kuwa mashairi.
1. Hapa tunaona kuna nyumba ya balaza na "Mzee wa Siku," ni hekimu.
    - a. Unyeupe was nguo na nwele zinazimamia utukufu wake, Mat. 17:2.
    - b. Moto kutoka kiti cha enzi inasimamia hukumu ya haki; matyri ya kiti cha enzi yanaonyesha haki yataendelea mbele bila kisuwizi, Amosi 5:24.
    - c. Mto wa moto inasimamia ghahadabu wa uungu.
  2. Piga chuku au tia chumvi manumbari ya kumi (10), inweka wazi matokeo haya yataokea mbele ya wanadamu wote.
    - a. Jeshi la mbinguni, wanaotumikia Mzee wa Siku ni mashahidi wa sheria.
    - b. Wanadamu wote watasimama mbele wake kwa hukumu.
  3. Wakati washiriki watakaa, vitabu vitafunguliwa na hukumu itaanza.
- B. Sasa tunaacha mbinguni na tunarudi duniani pamoja na mnyama wa nne.
1. Danieli anamtazama tu kwa makini, anashangaa maneno ya pembe ndogo ya kujivuna.
  2. Lakini wakati hukumu yake itapita, mnyama wa nne atauawa na maiti yake itatupwa kwenye mto wa moto inaowaka sana.
  3. Na wanyama wengine walioishi kwa sehemu tu pamoja na mnyama wa nne watapewa hukumu pamoja naye.
- C. Maono huu inapanda sana mbele wa kiti cha enzi cha Mzee wa Siku bad ya hukumu wa mnyama wa nne kumalizika.
1. Saa hizi Danieli anamwona mtu **kama** Mwana wa Adamu, ambaye ni kinyume na mnyama.
    - a. Neno kuu hapa ni "kama," anaonekana kama mwanadamu.
    - b. Lakini anaingia hapa wakati anapanda mawingu ya mbinguni, haya yanaonyesha huyu ni kubwa kuliko mwanadamu, Mdo. 1:9.
  2. Halafu Mwana wa Adamu anaongozwa mbele wa Mzee wa Siku.
    - a. Pale alipewa mamlaka na nguvu zote zilizotamika na wanyama wanne, Mt. 28:18.
    - b. Pale watu wa mataifa yote walimwobudu kama pembe ndogo ilitamani, Mt. 28:18-20; Mdo. 10.

## III. Kutafisiri ya Ndoto.

- A. Danieli alisikia vibay kuhuhu yale alishaona, 15.
1. Moja alisimama pande ya Mzee wa Siku; yana maana gani?
  2. Alimjibu Danieli kwa kusema, kwamba wanyama wanne ni ufalme nne, yatatoka na kuanguka mbele ya ufalme wa milele.
  3. Hapa ndoto ya Danieli ni sawa ya ndoto ya Nebukaneza.
- B. Sasa Danieli alitamani kujua kuhusu pembe ndogo ya mnyama wa nne.
1. Tunaona pembe ndogo alitisha zaidi kuliko mapembe mengine.
  2. Pembe ndogo ikafanya vitu na watakatifu, na ilionekana kama pembe itashinda.
  3. Lakini, katika hekima ya Bwana akiona muda imefika atatangaza mwisho wa pembe na kuokoa watakatifu.
- C. Aliyekua naongea hapa alieleza mnyama wa nne ni ufalme wa nne atavamia ulimwengu nzima.
1. Mapembe makumi yanasimamia wafalme kumi, 24.
    - a. Kwa kuwa haya yameandikwa katika hali ya ufunuo (apocalyptic), wengine wanaamini "mapembe kumi" yanasimamia jinis Rumi itatawala wote kwa nguvu na mamlaka.

- b. Wengine wanaamini "mapembe makumi" ni wafalme waliotawala kutoka kuzaliwa ya Yesu mpaka Yerusalemu ilianguka:
  - 1) Augustus, Tiberius, Caligula, Claudius, Nero, Galba, Otho, Vitellius, Vespasian, na Tito.
- 2. Bada ya hawa huyu pembe ndogo atatokea ku kungoa pembe au wafalme watatu na atakuwa mjadhambi (kufuru) mkuu.
  - a. Ataongea kinyume na Mungu na atatesa watakatifu.
  - b. Kuna mafundisho ya aina mbili ya jinsi ya kutafsiri "pembe ndogo."
    - 1) Fundisho ya kwanza inaona dini ya serikali ya Rumi kuwa pembe ndogo, kwa kuwa waliabudu wafalme (emperors) juu ya Mungu.
    - 2) Fundisho ya pili inaona mfalme Domitian kuwa "pembe ndogo". Ndiyo yeye alianza mateso ya watakatifu iwe sheria ya ulimwengu nzima. Na yeye ni mfalme wa kwanza tangu Caligula, kudai yeye ni "Mungu," 24, na aliamini kabisa.
- 3. Kutambua mapembe waliongoa na pembe ndogo ni vigumu lakini kujua kabisa ni nani siyo muhimu sana.
- 4. Pointi kubwa ni watakatifu wataumia kwa sababu ya pembe ndogo kwa, "Muda, mamuda na nusu muda," 25.
  - a. 3 ½.
  - b. Ni nusu ya 7, saba ni numba ya uungu wa milele, nguvu yote na ukamilifu.
  - c. Kwa hiyo 3 ½ inasimamia kitu cha muda, dhaifu na kuweza kukosa.
    - 1) Numba pia inapatikana katika kitabu cha Ufunuo, na maana yake ni muda iliopangwa na Mungu, na siyo milele.
  - d. Kwa kusema pembe ndogo atatesa kwa kipindi cha 3 ½ maana yake ni kwa muda iliopangwa na Mungu, halafu hukumu juu ya pembe ndogo itatokea.
- D. Mtafsiri wa Danieli anaendelea kusema wakati Mzee wa Siku atafunga hukumu, basi pembe ndogo itatharibika kabisa, bila kurudi, hukumu wake ni ya milele.
  - 1. Wakati ule, ukku, nguvu na enzi itingia katika mikono ya watakatifu, mali ya Mzee wa Siku.
  - 2. Kwa maana Ufalme wa Mzee wa Siku itadumu kwa milele.

## Daniel 8

### Maono ya Daniel ya Kondoo Dume na Beberu

#### I. Historia na Uandishi wa maono.

- A. Daniel aliweza kuona haya katika mwaka wa tatu wa Belshaza (546), miaka mitatu baada ya ngozi ile katika sura ya saba.
  - 1. Kwa wakati huu alikuwa anaishi Shushani mji mkuu wa Uajemi, pamoja na ukweli kwamba aliishi Babeli.
  - 2. 546, Ulikuwa ni mwaka ambao Uajemi iliipiga falme ya Lydia katika Asia ndogo, akijiimarisha mwenyewe kwa upande wa mashariki na kuhakikisha uharibifu dhidi ya Babeli.
  - 3. Ono hilo inahusu, "muda ya mwisho," na "mambo ya badai," 26.
    - a. Kwa kuangalia na kusoma ono hilo, tunaona kuwa linahusisha tawala mbili za uajemi na Uyunani zilizofuata Babeli, Uajemi halafu Uyunani.
- B. Mtindo na jinsi lilivyo ono hili kama ufunuo, lakini na ufafanuzi humo humo kwenye habari.
  - 1. Hii inafanya maono haya kuwa kama chanzo katika kuelewa asili na utendaji wa maono katika fasihi za Kiebrania.
  - 2. Mfasiri wa ono hilo ni Gabriel, Lk. 1:19, 26.
  - 3. Lugha iliyotumika ni Kiebrania.

#### II. Ono na Maelezo yake.

- A. Mwanzoni, Daniel anaona mwana kondoo mume upande wa mto Ulai kule Susa.

1. Pembe mbili ni mataifa mawili yaliyoungana.
  2. Mede lilikuwa taifa lenye nguvu ulimwenguni, na sasa Uajemi nayo imeingia na kuwa Mshiriki mkuu ili kuimarisha biashara yao.
  3. Kusogea kwa kondoo dume katika upande wa Mashariki kuelekeza Kasikazini, Kusini na Magharibi inaoyesha uelekeo kamili wa Uajemi katika kuzipiga tawala zingine.
- B. Tena Daniel akaona Mnyama wa pili, Beberu mwenye pembe mmoja yenye nguvu, ilijitokeza katikati ya macho yao.
1. Beberu ni kiwakilishi cha Uyunani, pembe ni mfalme waa kwanza wa Uyunani, Alexandra III.
  2. Kujongea kwa beberu kutoka upande wa Magharibi kuelekea Mashariki pasipo kugusa ardhi inaonyesha ushindi wa haraka dhidi ya watu.
    - a. Alikwenda kutoka makazini yake kuelekea India kwa muda wa miaka 11 tu ! (334-323 K.K.).
    - b. Ni kama vile beberu alimshutumu kondoo dume, akaanza kuvunja nguvu zake na kumkanyaga hadi chini na kufa, ndivyo alivyofanya Alexandra mnamo mwaka 331 dhidi ya utawala wa Uajemi.
    - c. Kama vile pembe kubwa ya Beberu ilivyovunjika mbali na nguvu zake ilizokuwa nazo, ndivyo ilivyofanyika kwa Alexandra aliyefariki mwaka 33 na ufalme wake Ukagawanyika.
  3. Pembe nne zilizokuwa badala ya pembe kubwa, ndiyo alivyofanya Alexandra katika utawala wake. Waliweza kugawanya ushindi miongoni mwao, (22).
    - a. Ufalme wa Ptolemy, uliokuwa upande wa Alexandra, Misri.
    - b. Utawala wa Selucis, uliochukua Antiokio Shemu.
    - c. Yuda ilikuwa katika ya tawala hizi na ingeweza kusukumwa nyuma na mbele kw amuda wa miaka mingine mia moja hamsini.
    - d. Katika kipindi hiki kilichoshududia tawala lenye nguvu ya Helleniki kutoka Uyunani, Ilibidilisha taratibu za taifa la Kiyahudi.
- C. Swala kubwa kabisa katika maono haya ni kusitawi kwa pembe ndogo mbali ya zile pembe Nne, 9.
1. Hii inawakilisha Antiki IV (Ephiphane) kutoka nasaba ya kifalme ya Seleuci aliyetawala kutoka 176-164 K.K.
  2. Katika ono la Daniel, inaonekana hii pembe kam ndogo lakini ikakuwa hata kuwa na nguvu dhidi ya tawala za Kusini, Mashariki na "nchi nzuri."
    - a. Antiochus alioneka kiharibu Ptolemier na kuipiga Misri.
    - b. Ijapokuwa Yuda ilikuwa chini ya Seleucids kwa kipindi hicho lakini ilionyesha huruma kwa Ptolemies kwa sababu ndio waliosaidia Yerusalemu na kupewa hadi yao.
    - c. Wakai huu Antiochus alikuwa ametafuta mtu wa kumweka katika ofisi ya Kuhani Mkuu aliyekuwa ni mwana siasa wa Kiyahudi.
  3. Kwa jinsi pembe ilivyostawi, ikaongezeka na kuwa na majivuno hata "Majeshi ya Mbinguni" na "kuziangusha hata nchi na kuzikanyaga."
    - a. Antiochus aliwatesa Wayahudi siyo kwa vile aliwachukia isipokuwa kutoka na upendo wake kwa Helleniki, aliwataka Wayahudi wote kufuata tamaduni ni dini za Kiyunani.
      1. Kuhani mku Jason (Jina la Kiyunani) alitafuta mahali pa maonyesho (ukumbi) katika Yerusalemu, palipokuwa mahali pa kufanyia mambo machafu yasioyoadili kwa wakati michozo ilipokuwa inaendelea.
      2. Muda si mrefu ukuhani ulikuwa umesahaulika pamoja na huduma za kifalme na kugeukia maonyesho na michozo mbalimbali.
    - b. Siyo Wayahudi wote waliokuwa wanafurahi mtindo wa maisha wa Wayunani, na hii ikasababisha kuwepo kwa mtengano kati ya wale waliotaka

kudumisha mila zao na wale Wayahudi wa Kiheleniki.

1. Wale waliounga mkono Helleniki (Wayahudi) walifurahia ulinzi na fadhira za Antiokus lakini waliponga maelfu ya waliuawa.
  2. Migawanyiko hii kw namna nyingene ndiyo ilijulikana kama Mafarisariyo na Masadukayo.
- c. Manukuzi kuhusiana na "kuangusha chini" na "kukanyaga" ya Wayahudi ni adhabu ambazo Antiochus aliwapa wale ambao walikataa kutii njia zake.
4. Pembe ikaoneka kuwa na nguvu kama "Mkuu wa Majeshi" na kumwondolea patakatifu pa hekalu na sadaka za kila siku.
- a. Antiochus ubini wake ni Epiphanes ikiwa na maana ya "Mungu aliyejidhihirisha" lakini adui zake walimwita Epimenes, "Mtu alilyechanganyikiwa."
  - b. Mnamo mwaka 168 K.K. alishindwa vikali na Wamisri, alipokuwa anaudia naye alimalizia hasira yake kwa Wayahudi. Alipofika aliwasaidia Ptolemies.
    1. Aliondoa dini zao, na kuwa ni kisa kitahili, pia akasema ni kosa kuwa ana kitu kitakatifu, wala kuadhimisha sikukuu na mateleo.
    2. Alidhirisha hekalu la Yerusalemu kwa kutoa matoleo ya nguruwe kwa Zeus juu ya madhabahu. Tena alichukua mchuzi pamoja na nyama na kumwaga katika vyumba vitakatifu kwa ajili ya Mungu.
- D. Mwisho wa ile pembe ndogo unaonekana kati mstali wa 25, "Ataharibiwa siyo kwa nguvu za mtu".
1. Mnamo mwaka 167. K.K. Uasi dhidi ya Antiokus ulianza wakati afisa Seleucid alipojaribu kumweka Matathiasi kuw akuhani mkuu wa kuota dhambi kwa Zeus na afisa huyo aliuawa.
  2. Ijapokuwa Matathiasi aliuawa lakini uasi ukawa umeanza, na watoto wake walichukua uongozi hasa Yuda aliyelitwa "Makabayo" kwa maana ya "Nyundo."
  3. Waasi wa Makabayo wakaenea haraka hata Yuda, pamoja Wayahudi waliopogana vita vingi dhadi ya utawala wenye nguvuwa Shemu.
  4. Baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyochukua mika mitatu, nguvu za Antiochus zikaondolewa kutoka Yuda.
    - a) Hekalu likasafishwa na kuwekwa watu tena 25/12/165 K.K., Yn. 10:22.
    - b) Wakawa na uhuru kwa mika mingine 100.
  5. Antiochus akawa amepata utisho kwa kushindwa katika vita hivi kiasi cha kuchanganyikiwa na kufa mwaka uliofuata.
- E. Maumivu na mambo mabaya yaliyofanywa na pembe yamefupishwa katika (12) ilifanikiwa ktika kila kitu ilichofanya, na ukweli ukashushwa.
1. Mstali 13, Kiumbe cha Mbinguni kiliuliza ni kwa muda gani uchafuzi wa hekalu utakoma na jibu likawa ni nyakati za asubuhi na jioni 2,300.
    - a) Hekalu lilifunguliwa tena baada ya miaka 3 na siku 10.
    - b) Nyakati asubuhi na jioni 2,300 ni hesabu nyingine ikimaanisha kipindi fulani cha muda (wakati uliogawanywa, 2,300 ni kama miaka 6, na miezi 3 ni kama wazo lingine la miaka 7.

## **Daniel 9 Sabini "Saba"**

### **I. Historia Na Ufafanuzi Wa Kiuandishi.**

- A. Sura ya 9 iko katika tarehe za utawala wa Daniel wa uzao wa Wamedi aliyetawazwa juu ya miliki ya himaya ya Babeli.
  1. 539 K.K. mwaka ambao himaya ya Babeli iliangukwa na Koreshi muajemi.
  2. Kuna miaka kati ya sura ya 8 na 9.
- B. Katika kusoma maandiko ya Yerusalemu, Daniel sasa aliweza kujua wakati wa Wayahudi kurudi tena Yerusalemu, Yer. 29:10, 25:11.

1. Alitambua kwamba miaka 70 ya kipindi cha kukaa utumwani kilikuwa karibu kwisha.
  2. Kuna namana tata ambazo watu hutumia kuhesabu miaka 70.
    - a) 609 - 539 K.K- Baada ya kifo cha Yosea mfalme na baada ya Yuda kupoteza uhuru kwa Misri mpaka wakati wa mfalme wa Uajemi Koreshi kuamuru kurudi kwa Wayahudi na kujengwa mji wa Yerusalemu na hekalu lake.
    - b) 606 - 536 K.K- Kutoka Babeli klushinda Misri na walipochukua Yerusalemu, na kuchukua kundi la kwanza kwenda uhamishoni mpaka kumalizika kujengwa kwa hekalu na madhabahu yake n akufanyika kwa sadaka ya kila siku.
    - c) 586 - 516 K.K - Kutoka wakati wa kuharibiwa kwa Yerusalemu na hekalu lake mpaka wakati wakuachiwa kundi la kwanza la Wayahudi mapka wakati wa kumalizika kwa ujenzi wa mwisho wa hekalu.
  3. Kama Daniel alielewa miaka 70 ya utabiri wa unabii wa Yeremia kuwa ulikuwa unatimia wakati wa mwaka wa kwanza wa utawala wa Dario, basi atakuwa amechukua hesabu ya kipengele cha "a".
  4. Hata hivyo, kwa mtazamo wetu hakuna mojawapo ya hesabu ya hapo juu, inayoonekana kwamba ni bora zaidi au siyo sahihi kuliko nyingine.
- C. Sura hii imeandikwa naman mbili za kiuandishi wa namna fulani.
1. Ufafanuzi na Sura ya Daniel iko wazi.
    - a) Kuna toba binafsi na toba ya shambi ya taifa. 4-14.
    - b) Hii inafuatia ombi la msamaha na ombi la kujengwa upya kwa Yerusalemu na hekalu lake, 15-19.
    - c) Sura inatolewa katika unyenyekevu uhakika "Hatukutolei maombi yetu kwa sababu ya haki yetu lakini kwa sababu ya rehema zako nyingi." mst.18.
  2. Mungu anajibu maombi ya Daniel katika malaika Gabriel ambaye anamtembelea Daniel.
    - a) Si kwamba tu Mungu alikubali ombila Daniel, pia alimfunulia jinsi atakavyofanya.
    - b) Alimwonyesha kwa njia ya ufunuo.

## II. Sabini "Saba".

- A. Daniel alikuwa bado anaombi wakati Gabriel alipokuja kweke katika gari lake. Maana yake ni kwamba Mungu hakukawia kumjibu maoni yake.
1. Hii ilitokea wakati wa saa 12 jioni wakati wa muda wa kuto sadaka, Hes. 28:6, 21.
    - a) Hakuna sadaka inayotolewa kwa muda wa miaka 47, lakini muda wa kutoa sadaka bado ulikuwa unakubukwa.
    - b) Maono yalionyeshwa ylikuwa yanahusu kuumdwa upya kwa taifa la Yuda, Kujengwa upya kwa jengo la hekalu, na kuanza tena kutoa sadaka ya kila siku.
    - c) Pia ilihusu kwisha kabidsa kwa sadaka izo na kutolewa sadaka tukufu kwa watu wote.
    - d) Kwa hiyo muda wa maono, unaonekana kwamba umehesabiwa na kupangwa kwa kuhakikisha taarifa ya maono.
- B. Gabrieli anafafamua kwamba mpango wake ni kumpa Daniel hekima na uelevu kuhusu yale ambayo alikuwa akiomba. Kipindi cha miaka sabini "saba" kimeamriwa, 24
1. Tafsiri nyingi hutafsiri maneno haya isivyo majuma sahihi ni "sabini "saba".
  2. Mfano mwingine wakazi ya namba katika mfumo wa maono.
    - a) Namba saba - ni alama ya ukamilifu na utimilifu wa kimungu na namba 10 ni alama ya utimilifu wa kibinadamu.
    - b) Tafsiri ya jumla ya sabini "saba" ni hii kwamba Mungu alikuwa katika mpango wa kuonyesha kazi zake kuu katika ulimwengu wa binadamu kwa

- ukamilifu - kwa namna ambayo ni ya kipekee kwa taifa la Wayahudi.
3. Maono yanahusu matukio na katika mtiririko wake.
    - a) Hakuna ratiba iliyofichwa katika sabini "saba".
    - b) Ufahamu wa namna hii, ni katika faida katika Agano Jipya na kuwa na uelevu wa Ki-Biblia.

### III. Hakika Ya Sabina Saba.

- A. Katika jibu la Mungu kwa maombi ya Daniel, Gabrieli anataja vita sita ambavyo vitaisha, kamili au kamilika au kutimizwa katika kipindi cha sabini saba.
  1. Hivi vinaoneka vizuri zaidi kukaa pamoja katika jozi tatu zinazohusiana na ukamilifu.
    - a) Upotovu utaisha na dhambi itaisha, 24.
    - b) Unyonge utaondolewa, haki ya milele itatawala, 24.
    - c) Maono na unabii utafungwa na Patakatifu Pa Patakatifu patatolewa wakfu.
  2. Katika kuelezea ni kwa namna gani sabini saba itavyokuwa, Gabrieli anagawa sabini saba katika vifungu vitatu, 25.
    - a) Sabini "saba" itakwisha katikati ya kuamuru mamlaka ya kujengwa kwa Yerusalemu na kukamilishwa wakazi hiyo.
    - b) Kutoka kwa wakfu wa kumalizika kutoa wakfu kwa vitu sitini na vyomgo vya patakatifu pa - patakatifu. "saba" wakati ambapo mpakwa mafuta atakomeshwa atakuwa hana kitu.
    - c) Vifungu hivi vyote vinaonekana tu kuwa maandalio ya tukio mahususi la sabini "saba" ambapo mkakwa mafuta atahakikisha/atafanya Agano na watu wengi.
- B. Daniel aliomba msamaha na kutegenezwa upya kwa taifa la Israeli mji wa Yerusalemu na hekalu la Mungu.
  1. Kwa mtazamo wake, Danieli inaonekana alikuwa anategemea kufanyika upya kwa taifa la Israeli katika karne ya mwisho ya sita au katika mwanzo wa karne ya 5, kuwa majibu ya maombi yake.
  2. Maono kwa hakika yanasisitiza sabini "saba" kama kipindi muhimu ambacho matakwa ya Mungu katika ulimwengu yangekamilika.
  3. Mpakwa mafuta, sio taifa la Israeli ni kiini cha kuhusika katika wiki ya saba.
    - a) Kwa kejeli, taifa la Israeli pamoja na mji wa Yerusalemu na hekalu lake, kwa yakini inaonyesha kwamba utaharibiwa tena katika wiki ya saba.
    - b) Israeli pamoja na tahasisi ya Agano la Kale kwa hakika vilichagia mpango wa Mungu wa wokovu. Lakini wokovu na vitu hivyo havikuwa mapacha wanaofanana, na wala hivyo havikuwa mpango wa wokovu.

### IV. Fafanuzi Ya Sabani "Saba".

- A. Mtiririko wa vitu vitakavyofanywa wakati wa kipindi cha sabini "saba."
 

Vinatoa kifungu na uhakika unaohitajika katika ufufuzi wa maono. (24)

  1. Upotovu na dhambi vitakomwshwa, Rum.8:3.
  2. Malipo ya ubaya yatatolewa na haki ya milele itadumu, 2 Kor. 2:21.
  3. Maono ya unabii vitafungwa mpaka kuwekwa kwa 'Patakatifu Pa Patakatifu' itawekwa wakati Yesu akitimiza unabii wote, Ebr. 1:1-2.
- B. Hii inatupa ufahamu wa kutosha katika kujenga mtiririko wa kutiza maono ya Sabini "saba".
  1. "Saba" ya kwanza inaanza kwa Cyrus kuamuru kujengwa upya kwa Yerusalemu (539), na hitimisho kwa kumalizika kwa ujenzi wakati wa kipindi cha Nehemia (440 K.K).
    - a) Kitabu cha Ezra na Nehemia kinatupa uhakikisho wa uhakika wa kauli ya Gabrieli kwamba mji ungejengwa kipindi cha dhiki.
  2. Ifuatayo "saba" 62 inaendana na utimilifu wa kujengwa kwa Yerusalemu na kipindi cha mwisho wa "mpaka mafuta" Yesu ambaye Mwisho wa maisha yake ya duniani uiisha katika msalaba.
  3. Mwisho "saba" utahusisha muda unafuata kipindi cha masihi (Mpakwa



mafuta).

- a) Haya 26 inasema " maisha" baada ya 62 (majuma saba) atakuwa amaekataliwa mbali na atakuwa hana kitu.
  - 1) Kipindi hicho "watu wa mtawala" watakuja kuharibu Yerusalemu na hekalu lake vita ambayo itaendelea mpaka taifa la Israeli litakapoharibiwa kama vile limechukuliwa na mafuriko.
  - 2) Vipindi hivyo vilitokea wakati wa kusulibiwa kwa Yesu na matokeo ya kuharibiwa kwa Yerusalemu katika mwaka wa 70 B.K.
- b) Aya ya 27, inasema, masihi atafanya Agano na watu wengi kwa saba moja (Juma moja au siku saba).
  1. Katika ya saba (Juma moja) atakaomesha sadaka na dhambi na mahali pake litasimama chukizo la uharibifu ambao litasababisha kutengwa kawa hekalu utakaodumu mpaka wakati wa uharibifu.
  2. Hivi vilitokea na kutimizwa katika kuazisha Kanisa na katika kuaribiwa kwa hekalu na Rumi.
- c) Aya hizi zinaonekana kuonyesa matujio haya katika mkingamo
  1. Katika mtizamo wa Ki-Binadamu, inaonyesa kwamba Masihi ameuawa na ufalme wake umwchukuliwa na wakati huo mji wake na hekalu limeharibiwa.
  2. Ukweli wa Ki-Mungu (Wakiroho) ni kwamba, kofo cha mahi ni kufanyika kwa Agano Jipya na watu wote.
  3. Kwa hiyo mwelekeo unaendelea ambapo Mungu anatumia nguvu mwisho wa matakwa yake katika ulimwengu wa watu.

### **Danieli 10**

#### **Maono ya Danieli Mtu Mkuu**

#### **I. Utangalizi**

- A. Sura ya 10 - 12 inahusisha maono ya kitu kimoja, na yamegawanyika katika sehemu tatu, na kwa ujumla huwa yanachanganya watu.
  1. Sura ya 10, kumeandikwa matukio ambayo yanapelekea katika maono mahususi, ambayo yapo katika sura ya 11, sura ya 12 inachukua namna ya hitimisho la maono na mwitikio wa Danieli
  2. Aya ya kwanza sura ya 11 inapaswa ihusishwe na sura ya 10, wataalamu huona kwamba ni kama kamilifu ya sentensi inayoanza katika mstari ya 10:21b
  3. Aya nne za kwanza za sura ya 12 bila shaka iko pamoja na maandiko ya sura ya 11, ambayo yanatengeneza kilele cha maono kwa undani mwisho ni furaha kwa hiyo kileleni.
- B. Sura hizi huonyesha mfuatano wa maono ambayo yanaanzia sura ya 7 katika mfumo wa mantiki na hitimisho yakinifu, au hitimisho muafaka.
  1. Sura ya saba maono ya wanyama wanne, inaweka historia ya utangulizi
 

wa siku za mwisho za Mungu kuondoa uhusiano wake na taifa la Israeli.
  2. Sura ya 8, maono ya kondoo na mbuzi, yanaelezea kupotoka kwa Wayahudi kimaadili na kiroho kulikosababishwa na watu wa kigeni na adhabu zao.
  3. Sura ya 9, maono ya sabini "saba" inatabiri wayahudi kumkataa masihi
 

na kufuatia kutengwa kwa Wayahudi na hekalu lao wanalojivuna nalo.
  4. Sura ya 10-2 maono ya mtu mkuu, anahakikishia na kuthibitisha wa kuokoa wanaoamini kutoka katika dhiki na kufa kwa jamuhuri ya Wayahudi.
- C. Maono yaliyomo katika sura hizi yanaanzia katika mwaka wa tatu wa Koreshi wa Uajemi, 536 K.K.
  1. Ilikuwa katika mwaka huo jamuhuri mpya ya jumuiya ya Wayahudi iliyoundwa upya ilipomalizika kujengwa pamoja na ujenzi wa madhabahu ya kila siku.
  2. Kwa kejel imaono haya yanonyesha mbele siku ambayo dhabihu na sadaka hizo

zitakomeshwa milele.

3. Tarehe ya maono haya kutokana na Koreshi mjemi, zaidi ya Dario Mmedi (Kama ilivyokatika sura ya 9).

## II. Maono ya Utangulizi.

- A. Sura ya 10 inaanza na Danieli kupata maono, na yaliyoelezwa yako katika namna isiyo wazi.
  1. Yanahusu vita kuu.
  2. Ilikuwa ni maono ya hakika itakayotokea.
- B. Taarifa sahihi ya maono Ilimwangaisha Danieli.
  1. Kwa juma moja alifunga akiomboleza waliokufa.
  2. Akaacha na kujiweka nadhifu.
  3. Vita aliyोजना mpaka ikamsababisha awe hivyo itakuwa sio nyingine bali ni ile ya nchi ya Yuda na Rumi kati ya mwaka 66 - 70 B.K., ambayo ilisababisha kupotea kwa nchi ya Wayahudi.

## III. Mtumwa wa Uungu

- A. Katika mwisho wa wiki tatu za kufunga, Danieli anatembelewa na anayefanana na mtu, lakini ni kiumbe wa asili ya kiroho.
  1. Amevaa kama mfalme.
  2. Muonekano wake wa kimaumbile unaonyesha kuwa yeye ni wa namna ya kimungu, mwenye utukufu usiokaribiwa, mwenye ufahamu wa juu, nguvu na mamlaka.
  3. Huyu mgeni wa ajabu, anatabiri na habari ya mwisho ya maelezo ya kushuka kwa Yesu katika utukufu, kama alivyoonekana kwa Yohana katika kisiwa cha Patimo, (Ufu. 1:13-16).
- B. Danieli na wenzake walikuwa katika hofu wakati mtu mkuu alipowatokea.
  1. Wenzake wakakimbia, lakini Danieli labda kutokana na unyonge wa uzee wake na alivyokuwa amedhoofika na kufunga, alikaa kusikiliza maneno ya mgeni wa ajabu.
  2. Mtu alipoanza kuongea mtetemo wa sauti yake ulisababisha Danieli kuhema kwa hofu, 9.
  3. Mtu huyo alimgusa kwa vitanga vya mikono yake, halafu akamhakikishia Danieli kwamba amekuja kwake na habari kutoka kwa Mungu, kwa hiyo asihofu kitu chochote, 10.

## IV. Mapigano Mbinguni.

- A. Maelezo yake mtu huyo kuhusu kuahairisha kwa kuwepo kwake inawezekana yalieleweka kwa Danieli lakini kwetu sisi ni fumbo.
  1. Kiu ya Danieli kuelewa na unyenyekevu wake mbele ya Mungu imeonekana. Huyu aliyetumwa ilikuwa ni kwa ajili yake Danieli.
  2. Kuwepo kwake kumedhihirisha kwa sababu mkuu wa ufalme wa Uajemi amenizuia kwa siku 21(siku sawa sawa na Danieli alizotumia kufunga), 13.
  3. Lakini kwa kusaidiwa na Michaeli mmojawapo wa mkuu wa mbele na hivyo akaweza kuleta habari ya majibu ya Mungu kwa Danieli.
- B. Utambulisho wa Mikaeli, ambaye allitokea katika maandiko ya Danieli, Yuda na ufunuo tu, yanaweza kutupa msingi wa kufafanua baadhi ya vipengele vinavyosumbua katika haya ya 12 - 13.
  1. Danieli rejea zinamtambulisha kama mkuu.
    - a. "Mmojawapo wa mkuu wa mbele," 10:13.
    - b. "Mkuu wenu (wa Danieli)," 10:21.
    - c. "Jemedari mkuu ambaye huwalinda watu wako," 12:1.
  2. Yuda 9 inamwita "Malaika Mkuu", inamwonyesha katika kushindana na Shetani juu ya mwili wa Musa.
  3. Katika Ufunuo 12:7, anaonyeshwa kama kiongozi wa malaika dhidi ya malaika wa Shetani.
  4. Kutoka katika aya hizi chache tunaweza kupata hitimisho la kutusaidia.
    - a. Katika kifungu hiki, neno "mkuu" linaonekana kama aina ya malaika.
    - b. Malaika wa haki na malaika wa shetani wanapingana.

- c. Kuna ngazi za vyeo katika malaika.
  - d. Mikaeli anaonekana kuwa na cheo cha juu sana, kama malaika mlinzi.
- C. Tunachoweza kukiona kuhusu mapigano katika mistari 12-13.
- 1. Sambamba, mapambano yapo pia ndani ya nafsi Danieli katika maisha yake, kwa sababu kila akiangalia anaona haki ikiwa inakuwa na vipingamizi vya nguvu za uovu (Shetani).
  - 2. Habari hii inampa Danieli matumaini baada ya kujua kwamba Mungu atashinda.
  - 3. Inaonyesha kwamba watu wa haki hawajaachwa peke yao katika mapambano dhidi ya uovu (Shetani).
- D. Kama ndivyo au sivyo fungu hili litafafanuliwa kama maandiko yanavyoelezea utawala wa kimalaika, ambao unatufungua maswali.
- 1. Kwa hakika, malaika wa Mungu na malaika wa Shetani wanapigana vita ya kiroho, ambapo malaika wa Shetani wanataka kuharibu mpango wa Mungu kwa watu wake.

#### V. Asili ya Maono ambayo yataonyeshwa.

- A. Baada ya kuelezea kuchelewa kwake kuja, mgeni wa Danieli (Gabrieli) anakuwa yuko tayari kutoa taarifa.
- 1. Amekuja kuelezea kitu gani kitatokea kwa watu wake katika siku za mbele, 14.
  - 2. Kama maono ya kondoo na mbuzi, ina maana kidogo kwa watu wa wakati wake, lakini vitu hivi ameonyeshwa kwa faida ya Danieli, kwa sababu anaguswa na yatakayotokea mbeleni kwa watu wa Israeli.
  - 3. Mwisho wa maono, Danieli tena anaambiwa kufunga ufunuo mpaka "siku za mwisho" (12:4; 8:26).
- B. Kwa upande wake, Danieli hana uakika kwamba anataka kuogopa kuambiwa kitu ambacho mjumbe amekuja kumwambia.
- 1. Kwa kkuwa ameishapata maono ya kwamza, anakuwa hana uhakika kwamba moyo wake uko tayari kusikia habari mbaya tena.
  - 2. Mjumbe anamuhimiza kuwa na nguvu na amani alafu anamgusa Danieli tena nakumpa nguvu tena.
  - 3. Kwa hiyo Danieli yuko tayari kusikia.
- C. "Na sasa nitarudi ili nipigane na mkuu wa Uajemi; nami nitakapotoka huku, tazama, mkuu wa Uyunani atakuja," 20.
- 1. Tunaweza kukumbuka kwamba, katika mwaka wa 536 K.K., Himaya ya Uajemi haikuangushwa na Alexanda mpaka 332 K.K.
  - 2. Kwa hiyo, "haraka sana" hapa inamaana miaka 200.
- D. "...Lakini nitakuwambia yalioandikwa katika maandiko ya ukweli...., 21.
- 1. Kabla ya mtiririko wa matokeo, Danieli atakuwa anajua kila kitu kitakachotokea.
  - 2. "Maandiko ya kweli" hapa hayamaanishi maandiko ya Biblia.
    - a) Zaidi yanamaanisha, mpango wa kutimiza mapenzi yake katika historia ya mwanadamu.
    - b) Kwa mtazamo wa watu wasiomjua Mungu, kifungu hiki kinaweza kuleta maswali juu ya Mungu. Kwa sababu inaonyesha mkuu wa giza anashinda.
    - c) Lakini kwa kuangalia maandiko ya kweli inatufanya tuone kwa uhakika kuwa Mungu ni mshindi, na nguvu za giza haziwezi kusimama.
  - 3. Hii itakuwa ni faraja kwa Danieli kutokana na majibu ya Mungu kwa ajili ya uzuri wa Danieli.

### Danieli 11:1 - 35

#### Maono ya Danieli ya Mtu Mkuu (II)

##### I. Utangulizi:

- A. Paragrafu za vitabu vya zamani na vya kisasa zinatofautiana katika maana ya haya ya kwanza ya sura ya 11.
- 1. Mtazamo wa zamani unakazia katika mgawanyo wa sura unamfanya Dario Mmedi

- kuwa sababu ya ulinzi wa mjumbe.
2. Mtazamo mwingine, unaonekana katika paragrafu za kisasa unaona kwamba Mikaeli kama mpokeaji wa Ujumbe.
  3. Kwa vyovyote vile bila kujali mtazamo gani mtu anakubali, kiujumla. Historia ya mambo yaliyoonekana, ni namna ambavyo Mungu anatimiza matakwa yake katika ulimwengu.
- B. Hivyo, mjumbe wa Danieli ni kwa ajili ya kutabiri mambo ya matukio ambayo yangetokea miaka 600 ijayo.
1. Upana wa kihistoria wa maono unaanzia katika kipindi cha utawala wa kiajemi katika mashariki ya karibu (12:2).
  2. Mwisho wa maono ni kipindi “watapokuwa wamekwisha kuvunja nguvu za hao watu watakatifu” ... (12:7), kwa uhakika matukio ya kihistoria ambayo yanaonekana hapa, yataeleweka vizuri kwamba ni maono ambayo hayajafunguliwa.
  3. Matukio ya kihistoria yanatoa nguvu ambayo itatusaidia kufafanua maono; hivyo ufafanuzi wowote ule ambao utakwenda nje ya muda ambao "Nguvu za watakatifu zilivunjwa," utakuwa sio sahihi.
- C. Wakati tunasoma, lazima tuelewe akilini kwamba, sababu ya Danieli kupata maono ilikuwa ni kwamba aweze kuelewa vizuri sababu ya matokeo ya “vita kuu” ambayo aliona katika maono ya kwanza ambayo ilimfanya augue sana, (10:1-3).

## II. Mwisho wa mamlaka ya Uajemi.

- A. Mjumbe kwanza anamwambia Danieli kwamba, baada ya Koreshi, wafalme watatu zaidi watatawala. Kabla ya mfalme wa nne ambaye angesababisha mafarakano Uyunani.
- B. Waliomfuata Koreshi (alikuwa 529 K.K.) walikuwa:
1. Cambyses (529 - 522 K.K.)
  2. Smerdis (522) mtawala aliyetawala kama kaka yake Cambyses, na mrithi wa ufalme, kama alivyompindua Cambyses, utawala wake haukuchukua muda mrefu.
  3. Dario “Hystapes” (521 - 485) wakati wa utawala wake hekalu katika Yerusalemu lilimalizika.
  4. Xerxes I, (485 - 464), Ahasuero wa kibiblia, ambaye alimuoa Esta ambaye aliljaribu bila mafanikio kuwashirikisha Wayunani katika utawala wake bila mafanikio.
- C. Maelezo ya kuanguka kwa Uajemi kwa Alexander mkuu, baadae kugawanyika kwa himaya kwa wakuu wake wanne inaonekana kirahisi katika haya 3 na 4.
1. Japokuwa Xerxes alikuwa mfalme wa kwanza kusababisha mafarakano kati ya Uajemi na Uyunani karne nyingi zilipita wakati wa kifo chake mapaka wakati wa Alexander kuangusha himaya ya Uajemi kwenye miaka ya 334 K.K.
  2. Kipindi cha muda huu, wafalme wengine wanane wangetawala Uajemi.
  3. Chini ya mamlaka ya Alexander, Palestina iliunganishwa katika jimbo la Coele Syria.

## III. Yuda chini ya Ptolemies.

- A. Haya 5-35 inaonyesha mgogoro wa kushangaza kati ya Himaya mbili za Hellenistiki ambazo zilitokea kutokana na kuchukua mamlaka kwa Alexander.
1. Himaya ya Ptolemies, ambayo chanzo chake ni Misri, inaonyeshwa katika kitabu hiki kama ufalme wa kusini.
  2. Himaya ya Seleucid ambayo mji wake mkuu uko Shemu, imeonyeshwa kama ufalme wa kaskazini.
  3. Mtawala wa kwanza wa ufalme wa Shemu Seleucis wa kwanza “Nicator” alikuwa kwanza amekimbilia Misri kwa hifadhi wakati huo akiimaniha kurudi tena Shemu kwa kukusanya nguvu ya kuchukua Shemu. Yeye ni jemedari wa 5 ambaye alitwaa Shemu kuwa milki yake.
- B. Haya 5 - 13 inaelezea sababu ya matukio ya 320 na 221 K.K., ambapo

Palestina ilikuwa lasimi chini ya milki ya Ptolemies.

1. Taratibu “ustaarabu wa Kiyunani” kuingizwa katika utamaduni wa Kiyahudi kwa kipindi hicho, ilisababisha jamii kubwa ya Kiyahudi kuishi Alexandria.
2. Tukio lingine ambalo lilitokea wakati huo ilikuwa ni kutafsiri mabadiliko matakatifu

ya Kiyahudi kwenye lugha ya Kiyunani (Septuagint).

#### IV. Antiochus III

- A. Kitu muhimu cha kuzingatia katika vita kati ya Misri na ashuru ambayo ilitokea wakati wa utawala wa Antiochus III (mkuu) dhidi ya himaya ya Seleucid (223 - 187 K.K.) ni utawala wake katika haya ya 14-19 ya maono.
1. Kushinda kwa Seleucid katika Bania kulisababisha kuhamisha utawala kutoka Misri kwenda kwa Shemu haya 15-16.
  2. Japokuwa Antiochus alikuwa na nguvu za kuangamiza Israeli, hata hivyo kwa hakika aliwafanyia ukarimu na uvumilivu.
  3. Wakati wa kipindi cha utawala wake, ni ambapo Shemu ilipata mfarakano na himaya iliyokuwa inakuwa ya Rumi.
    - a. Katika kuepuka vita mbili mbili iliyokuwa mbele, Antiokusi aliozesha binti yake Cleopatra (siyo yule mashuhuri), kuolewa na Ptolemy (17), kama mahari alitoa jimbo la {Coele - Syria} ambapo hiyo ilitengeneza amani kati yake na Misri.
    - b. Akiwa hana hakika kuwa wamefanya amani na maadui wao wa Kusini, Antiochus alijaribu kudhibiti kijeshi dhidi ya Rumi, na akaendesha kampeni ya kumuondoa rumi katika kumiliki Asia ndogo na nchi ya Uyunani. (18a).
    - c. Baada ya muda fulani akashindwa kumkabiri rumi kutokana na vyombo vyake vya kivita, na akashindwa vita katika Thermopylae katika mwaka wa 191 na katika 190 (18b).
  4. Baada ya kushindwa, Antiokusi alilazimika kulipa fidia kwa Rumi au kuwa alitayarisha kushambuliwa na majeshi ya Kirumi.
    - a. Kwa hiyo alichagua kulipa fidia ambayo aliilipa kwa kuiba vitu kutoka katika mahekalu ya Ashuru na Uajemi (19a).
    - b. Hii ilisababisha kuondoa utukufu, na hii ikasababisha mapinduzi katika 187 ambapo Antiochus aliuawa (19b).
- B. Mstari ya 20, inatosha utawala mfupi wa Selsucis IV (187 - 175 K.K.).
1. Kazi yake kubwa kama mfalme ilikuwa ni kuwatoza watu kodi ili kulipa fidia iliyokuwa imeamriwa na utawala wa Rumi (20a).
  2. Kichekesho aliuawa na mtoza ushuru mkubwa kwa sababu za kisiasa katika mwaka wa 175 K.K.

#### V. Antiochus IV.

- A. Utawala wa Antiochus IV "Ephiphanes" 175 - 164, imeonyeshwa katika mistari ya 21 -35.
- B. Alikuwa kaka yake Sleucis IV, ambaye ni mrithi wake Demetrius I "Soter" ambaye alikuwa amefungwa Tome kungihea kulipwa fidia. Antiochus alichukua nafasi ya kuwepo kifungoni kuchukua ufalme mwenyewe (mstari 20-24).
- C. Kama tulivyokuwa tumeisha ona kabla, Antiochus alipenda kuunganisha jumuiya yote ya Kiyunani, na kuharibu utawala wa Ptolemaic Misri.
  1. Kati ya 171 - 168, Antiochus alivamia Misri.
    - a. Katika mwaka 170 alifanikiwa kufanya Misri yote isipokuwa mji wa Alexandria chini ya himaya yake. (mistari ya 25-27).
    - b. Alipokuwa akirudi nyumbani alipitia Yerusalemu kuwaadhibu waliokuwa wanakataa sera za kuwa chini ya Uyunani, alikukwepo kwa siku tatu, akatawala kwa vitisho, na akaacha sehemu kubwa ya mji ikiwa imechomwa na kuharibiwa na mamia ya Wayahudi waliuawa au walifanywa watumwa (mst. 28).
  2. Katika kampeni ya 168, ambapo ilionekana kama anakwenda kuuteka mji wa Alexandria, majeshi ya Rumi yalilweka upinzani na kumlazimisha kurudi nyuma (haya 29 - 30a) akiwa anarudi nyumbani alipolipiza kisasi kwa Yerusalemu kwa mara ya pili.
- D. Katika mawazo yake ya wazimu, Antiochus alildhamilia kufutulia mbali utamaduni wa

Kiyahudi (30b).

1. Katika mwaka 167 BC alitoa wakala wa kuaramisha dini ya Wayahudi vitu vyote vya Kiyahudi pamoja maandiko ya Kiyahudi yalifanywa kuwa jinai (haramu kisheria). (31a).
  - a. Halafu aliweka madhabahu ya Kiyunani katika Yudea nzima na kuamuru watu kutoa sadaka kwa miungu ya Kiyunani.
  - b. Mwenyewe alinajisi hekalu la Yerusalemu kwa kutoa sadaka ya nguruwe kwenye madhabahu ya dhahabu (31b).
2. Wakati ambapo wayahudi wengi kwa kuchukuliwa na mkumbo huo, na kuwa na woga, waliacha imani yao na kuanza kuambatana na ustaarabu wa kipagani wa Kiyunani, kundi la waaminifu walikazia kumtii Mungu na kuwa adui wa Antiochus mpaka kufa kwao (mst. 32 -35).
  - a. Kupigwa marufuku maandiko, ilihitaji kutambua maandiko kutoka katika maneno ya vitbu visivyoamuriwa (visivyo vya Mungu).
  - b. Hii ilisababisha vitabu vinavyoitwa “Apocrypha” vitabu hivi havihusishwi na kitabu cha Biblia, kwa sababu ni vya kibinadamu zaidi kuliko kiroho kidini, hivyo vilikuwa havina sifa za kustahili kuuawa kwa hivyo!
3. Katika 167 K.K., katika mji mdogo wa Wayahudi uitwao Modein, mtawala wa Shemu alijaribu kulamzimisha kuhani aliyezeeka kutoa sadaka kwa Zeus, ambapo hii ilisababisha mlipuko wa maasi dhidi ya utawala wa Seleucid, hii ambayo kujulikana kama Mapinduzi ya Makabayo.
  - a. Hii ilisababisha Antiochus kubadili sura ya kuwalazimisha Wayahudi kufuata upagani wa Kiyahudi na kutaka kufutilia mbali Wayahudi.
  - b. Lakini kabla hajafanya hivyo, aliuwawa katika vita katika Parthia katika mwaka wa 164 K.K.
  - c. Kutoka hapo wayahudi kwa mara ya kwanza baada ya miaka ya mamia, ilipata uhuru ulichukua karibu miaka mia moja.

### **Danieli 11: 36 - 12:13**

#### **Maono ya Danieli ya mtu mkuu - III.**

#### **I. Utawala wa Rumi:**

- A. Kwenye mstari wa 36, taarifa ya mjumbe inatokea kwa wakati wake baada miaka 100 mbele, wakati wa kumiliki kwa Warumi, baada ya kuiangusha Shemu na Palestina.
  1. Kipindi cha mpito kitakuwa lahisi kuonekana kwa sababu ya kafara na kujikuza kwa “mfalme na kufanya yanayompendeza tu” katika haya ya 36 inaungana na usemi huu mpaka haya ya 21.
  2. Hata hivyo mfalme katika haya ya 36, atafanikiwa kudumu mpaka wakati wa ghadhabu itakapotimia.
    - a. Huyu awezi kuwa Antiochus IV.
    - b. Wakati wa ghadhabu inaashiria “vita kuu” ambayo Danieli aliona katika maono ya kwanza (10:1).
    - c. Mfalme katika haya 36, hivyo ana maanisha “mtawala ambaye” alivunja nguvu ya watu watakatifu, 12:7.
    - d. Hii yote inamaanisha kuaribiwa kwa Yerusalemu na nchi ya Waisraeli katika mwaka wa 70 B.K. na Rumi.
  3. Kutambua mfalme na himaya ya Rumi inafanya maono haya yawe muhimu hata kwa wengine katika kitabu hiki, ambacho kinaonyesha kufuatana kwa utawala wa himaya kutoka himaya ya Babiloni kufuatia Uajemi, Uyunani mpaka Rumi (sura ya 2 mpaka ya 7).
- B. Kwa kuona kuwa mfalme sio mwingine na himaya katika aya ya 36 inamaanisha kidogo kwa upande wa mfalme wa kaskazini kutoka kwa himaya ya Seleucid, ambayo sasa anapewa mfalme wa Rumi, na hii kwa yakini inaendana sawa na ukweli wa kihistoria.
  1. Himaya ya Seleucid ilichukuliwa na majeshi ya Kirumi chini ya utawala Pompey

katika mwaka wa 64 K.K.

2. Kutoka kipindi hicho na kuendelea warumi, waliendesha vita kutoka kwa Shemu dhidi ya utawala wa Misri, kundi la himaya ya Alexander ambayo ilichukua muda na ikaangushwa ikiwa ya mwisho.
- C. Haya ya 36 - 39, inaelezea mfalme huyu kama atamwabudu Mungu wa nguvu na nguvu za kijeshi naye atafanya kama apendavyo katika kutimiza lengo lake la kutawala ulimwengu.
1. Dini ilitumika kama njia ya kukubaliwa na mataifa, kwa vile angeabudu miungu wa watu wowote wale ili kufanya wafurahi.
  2. Mfano wa hii Herode mkuu ambaye alikuwa kibaraka wa Rumi ambaye alitengeneza Hekalu kuwa kubwa ilikuwafanya wayahudi wamkubali, japokuwa alikuwa sio mtu wa dini au mtu wa maadili ya namna hiyo.

## II. Uvamizi wa Rumi kwa Misri na Palestina.

- A. Siku ya mwisho katika haya 40 inamaanisha mwisho wa Ptolemies na haya zifuatazo kwa usahihi zinaelezea uvamizi wa Rumi kwa Misri.
1. Mfalme wa Kusini, kwa wakati huu alikuwa ni Malkia wa Cleopatra.
  2. Wakati fulani, alikuwa hawala wa Julius Kaisari, na alimzalia mtoto wa kiume.
  3. Baada ya Kaisari kuuawa mwaka 44 K.K., aliolewa na Mark Antoni ambaye alikuwa akimshindania na mjomba wake Kaisari na mtoto wa kurithi Octavian kwa ajili ya madaraka katika Rumi.
- B. Akitumaini kufanya Misri kuwa kitovu cha utawala wa ulimwengu, Cleopatra alimshawishi Antoni kufanya mashambulizi ya kijeshi dhidi ya Octavian.
1. Octavian aliomba baraza la Rumi atangaze vita dhidi ya Cleopatra, bila kumjali Mark Antoni.
  2. Kwa hiyo, vita iliyokuwepo ya Octavian na Antoni. Ilikuwa sio vita ya ndani ya Rumi bali vita kati ya ufalme wa Kaskazini dhidi ya ufalme wa Kusini.
- C. Vita inayoonekana katika aya ya 40a ilipigwa na jeshi la farasi na Merikebu ni kuhusu vita.
1. Japokuwa Antoni alikuwa na jeshi lenye nguvu la nchi kavu na majini lilikuwa sio vyovyote kulinganisha na Rumi, alianguka katika tamaa ya Cleopatra akapigana vita ya majini na kushindwa.
  2. Baada ya vita hivyo vya Actium, Antoni na Cleopatra alijinyonga na Octavian akabaki kama mkuu wa Rumi asiyepingwa.
    - a. Vizuri umjue agustus Kaisari.
- D. Kufuatila vita ya Actium, jeshi la Rumi lilitoka Palestina na Misri (40b - 45).
1. Japokuwa wayahudi walimezwa na Rumi, mataifa jirani ya Wamoabu na Adomu na Waamoni hawakuwahi kuwa chini ya kinga ya Rumi kama Uyahudi (44).
  2. Pia, Rumi ilikuwa wakati wote inajihusisha vita na makabila ya Kijerumani upande wa kaskazini na Mashariki na hizi hazikuwahi kuwa chini ya Rumi, na zilikuwa tishio sana kwa himaya ya Rumi kuanzia wakati wote wa kipindi cha himaya hiyo. (44).
  3. Haya ya 45 itaelezea Rumi kutwaa Palestina na Yerusalemu nguvu zake zilikuwa zina uwezo wote wa kuharibu mpaka wakati wa kuisha kwake lakini ilikuwa imepangiwa mwisho wake.

## III. Majilio ya masihi.

- A. Sura ya 12:1-4 inaonyesha hitimisho la maono, maandiko yote yanayofuata yanaishia katika kipindi hiki.
1. Katika 10:14, mjumbe wa Danieli aliahidi “Itakuambia wewe kitu kitatokea kwa watu wako katika siku zijazo, kwa kuwa maono yanahusu siku za mbele zitakazokuja.”
  2. Sura ya 12 inatupelekea katika mfuatano wa himaya mpaka wakati wa utawala wa Rumi hadi kumiliki Uyahudi.
- B. “Wakati huo” anasema mjumbe, (wakati wa kumiliki kwa Rumi). Mikaeli, jemadari mkuu atasimama ambaye huwalinda watu wako.
1. Tumeishaona kuwa malaika Michaeli anaonekana kama mlinzi wa watakatifu wa Mungu (10:13, 21).
  2. Aliwahifadhi na kuwalinda watu watakatifu katika kipindi cha Uajemi na Uyunani walipokuwa chini ya mamlaka yao, hata wakati wa dhiki walizopata chini ya utawala

- wa Rumi, alikuja tena.
3. Kila aliyekuwa jina lake limeandikwa katika “kitabu” ataokolewa kupita (sio kutoka) katika dhiki hii.
    - a. Japokuwa “kitabu” hakijafafanuliwa wazi katika kitabu cha Danieli, dhana ya Mungu ni kitabu cha uzima, ambacho ndani yake kuna majina ya watu wake watakatifu kitakuwa kina uamuzi ambao ni sawasawa na Musa (Kut. 32:32, Lk. 10:20, Ufu. 20:12).
- C. Haya ya 2, inaonyesha bila shaka kama vile ni kidokezo cha hukumu ya mwisho lakini hata hivyo sivyo kulingana na haya ya 7.
1. Ufunuo ni neno la kawaida katika Agano la Kale.
    - a. Hosea aliita tendo la kuokolewa kwa Wayahudi kutoka uhamishoni kama kufufuka kutoka kaburini (Hos. 13:14).
    - b. Ezekieli anafananisha kuja kwa Masihi na baraka atakazozileta kama kuwafufua (kuwainua) kutoka kaburini, Eze. 37:11-14.
  2. Ufufuo katika haya haya ya 2, ni kutumwa kwa masihi kwa Waisraeli.
    - a. Baadhi watafufuka kwa ufufuo wa milele.
      - 1) Mwenye hekima ambaye atangaa kwa utukufu wa Mbinguni.
      - 2) Ni ambao watakaowaongoza wengine katika haki, ambao wataang’aa milele na milele.
    - b. Wengine watafufuliwa kwa aibu ya milele na milele.
- D. Daudi anaelekezwa afunge kitabu mpaka siku ya mwisho.
1. Siku ya mwisho, inatofautiana katika kitabu chenyewe kulingana na vifungu vinavyoonekana.
  2. Kwa hili inaonekana kuwa na maana ya muda wa kipindi cha uhuru kulichotokea baada ya mapinduzi ya Makabayo.
    - a. Kilikuwa ni kipindi cha kufurahisha sana kwa kizazi kipya cha Taifa la Wayahudi.
    - b. Kilikuwa ni kipindi kilichoambatana na mabadiliko ya kisiasa na kutokuwa na uhakika wa nyakati na haku ya baadae.
    - c. Kilikuwa kipindi hakika wayahudi walijihusisha na kusoma.
  3. Kufunga kitabu mpaka siku ya mwisho kungefuatia maandiko ya kiroho kuelezea au kuwa fafanulia maandiko watu ambao wangekuwa na wasiwasi na kuchanganyikiwa wakati huo.

#### IV. Hitimisho.

- A. Wakati ambapo maono na kitabu kinapomalizika, Danieli amuona mjumbe wa mbinguni juu ya mto, akiwa pamoja na ujumbe wa kimalaika wengine ambao walikukwa wamekaa pembezoni mwa mto.
1. Mmojawapo wa hawa akamuuliza mjumbe wa Danieli swali, “Itakuwa muda wa miaka mingapi hata mwisho wa mambo haya ya ajabu?”
  2. Jibu linatolewa kwa kiapo kikubwa, “Itakuwa wakati, nyakati mbili na nusu wakati.”
    - a. Kwa mara nyingine namba za ki-utabiri zinaonekana tena 3 ½ ikionyesha wakati mahususi ambao Mungu atatumia taifa fulani, watu au mazingira ya namna fulani kutimiza makusudi yake ya Kimungu.
    - b. Danieli anaambiwa mambo yatakayotokea katika mpangilio wa kalenda yakionyesha ni siku gani hasa haya yatatokea.
    - c. Anaambiwa tu siku ambayo nguvu za watu watakatifu zitakuja ndipo vitu vitakapotimia, (mst. 7).
      - 1) Lazima tuzingatie aya hii katika akilini mwetu tunapokuwa na mwisho wake wakati yote yatakapotimia na sio baada yake.
- B. Danieli kidogo amechanganyikiwa kwa ufunuo ambao sio dhahiri.
1. Kwa baadhi ya vipengele na maswali yanaachwa wazi kwa sababu ya kuisha kwa ghafla kwa maono.
    - a. Kitu gani kitatokea baada ya nguvu zao kuvunjwa?
    - b. Vipi kuhusu rumi, kwa kipindi cha muda gani wataendelea kudhuru dunia?
    - c. Vipi kuhusu watakatifu ambao wako chini ya uangalizi wa Michaeli.



2. Swali la Danieli ni kitu gani kinachoendelea au kitu gani kitafuata.
3. Mjumbe hajaamuliwa kujibu maswali haya kwa undani. Danieli lazima atakuwa katika fikira na yale ambayo ameyaona katika maono haya maawili.
  - a. Kinachoendelea ni kwamba, wenye haki watakuwepo siku zote kama vile wapotovu watakavyokuwepo.
  - b. Kipindi cha uonevu wa warumi katika siku 1,290 (II) yaani miaka 3 1/2 au "nyakati, nyakati mbili na nusu nyakati"
  - c. Baraka zilitangazwa kwa wale watakaovumilia mpaka siku 1,335.
    - 1) Ujumbe unaeleweka, kwa wale waamini kuwa waaminifu mpaka mwisho, watapata dhawabu.
- C. Kipindi cha muda ambacho kitabu cha Danieli kinaishia, ni hapo ambapo kitabu cha Ufunuo, ndipo kinapoanzia kuhusu nguvu ya rumi kwa hiyo kitabu cha Ufunuo kinaweka historia iliyokuwa imepumzika.

### **Danieli na Imani ya Miaka ya Elfu moja**

#### **I. Utangulizi.**

- A. Ufalme wa Mungu kwamba umeshaanzishwa au sivyo, hakuna kati kati!
- B. Wakristo kwa sasa wanaamini kuwa kanisa ndio ufalme wa Mungu.
- C. Wanashikilia imani ya kabla ya elfu moja wanadai kuwa kanisa liliwekwa badala ya ufalme wa Mungu, litadumu mpaka muda mahususi kwa ufalme kuanzishwa.
- D. Wenye imani hii, huchukua unabii wa ufalme wa Mungu na kuchanganya na lugha ya mifano (ya alama) iliyopo katika Ufu. 20, na hapa ndipo wanapopata imani yao hiyo.
- E. Imani hiyo inatokana na neno Premillennium ambalo linatengenezwa na maneno mawili yani pre-maana yake "kabla", Mille - maana yake "elfu moja", Annus - maana yake "miaka."

#### **II. Msimamo wa watu wa Imani hiyo.**

- A. Hukazia kwamba Kristo atakuja na kutawala miaka 1,000 ufalme wake ikamilika kwenye kipindi hiki.
- B. Imani hii inamfundisho ambayo yako katika mgawanyiko, na fundisho lililomashuhuri zaidi lakini lililokufa ni mgawanyo wa nyakati kabla ya miaka elfu moja (Dispensational Premillennialism).
  1. Imani hii hugawa historia ya wanadamu katika nyakati 7, ambazo ni vipindi vya tawala za falme mbalimbali.
  2. Wanadai kuwa tawala ya falme ya nne inawakilisha Rumi kama himaya itakayoundwa upya ambayo Yesu atarudi tena kuiharibu.
    - a) Kwa hiyo wanadai kwamba kuharibiwa kwa Rumi hakukufanyika alipokuja mara ya kwanza lakini utafanyika wakati wa Rumi mpya itakapoundwa upya na Yesu atakuja mara ya pili.
    - b) Kama hivyo ndivyo ilivyo, Yesu hakushinda sanamu lakini sanamu ilimshinda.
- C. Mtazamo wa imani hii siku hizi sio sawa hasa na mtazamo wa imani hii katika wakati mwanzo (asili ya Imani hii). Ila ni mchanganyiko wa Imani ya miaka kabla ya elfu moja kabla ya ufalme wa Mungu na ya mgawanyo wa nyakati wa vipindi vya tawala za falme (Premillennialism and dispensationalism).
  1. Wanaamini kuwa Mungu aliumba kwa siku sita na siku ya saba alipumzika.
  2. Kwamba Petro alisema kwa Mungu siku moja ni miaka elfu moja, 2 Pet. 3:8.
  3. Wanaamini kwa kufuata mtiririko wa uumbaji kwamba historia ya mwanadamu imegawanyika katika vipindi saba.
  4. Kwamba, kwa vile Mungu aliumba siku sita ya saba akapumzika, kwa hiyo baada ya siku sita miaka 6000 Yesu Kristo atakuja kutawala na kutengeneza ufalme wake katika miaka mingine 1000.
  5. Ni imani kubwa sasa hivi katika baadhi ya wafuasi wa imani hii (Premillennialist) lakini iko hatarini, kwa vile sasa tuko katika 2002, sasa Yesu yupo wapi?

### III. Jinsi ya kupinga uongo huu wa Premillennialism.

- A. Danieli (2).
1. Katika siku hizo Mungu atasimamisha ufalme wake na kuiharibu sanamu kwa milele.
  2. Aya ya 40 “ufalme wa nne”, lazima utakuwa umekuja 34 K.K. mpaka 476 B.K. ni wakati ambapo ufalme wa nne ulitawala ulimwengu.
- B. Kulikuwepo na ufalme ulioanzishwa wakati wa utawala wa Rumi?
1. Mat 3:2, 4:17; Mk 1:14.
  2. Mk. 9:1.
  3. Mdo. 1:1-4.
  4. Mdo. 2:1-4.
  5. Mat. 16:18-19.
  6. Mdo. 2:47.
  7. Kol. 1:13.
  8. Heb. 12:12.
  9. Ufu. 1:5-9.
  10. Yn. 1:5.
  11. Yn. 18:36.
- C. “Jiwe lilichongwa pasipo mikono ambalo lilipiga sanamu miguu yake ambayo ilikuwa ya chuma na udongo na kuzivunja katika vipande vipande,” 2:34.
- D. Ni nani aliyekuwa jiwe?
1. Mat. 21:42; Mk. 12:18; Lk. 20:17; Mdo. 4:11; 1 Pet. 2:4.
- E. Danieli 7, Mzee wa siku, mwana wa Adamu.
1. Mzee wa siku - Baba.
  2. Mwana wa Adamu - ni Yesu. Mt. 16:13; 16 - 17.
  3. Mwana wa Adamu alikuwa atolewe:
    - a. Utawala - soma Efe. 1:20-23
    - b. Utukufu - soma Yn. 17:4; Ebr. 1:1; Yn. 17:24.
    - c. Ufalme - soma Eze. 1:13.
      - 1) Mifano katika Lk. 19:12.
- F. Danieli 2 na 7 zinaonyesha wakati ambapo kipindi cha utawala wa Rumi, wakati ambapo “jiwe” lingepiga nguvu ya utawala ya ulimwengu.
- G. Kwamba ufalme wa Mungu yaani kanisa, lingetawala milele na sio kwa muda fulani tu, (hautaondolewa), Dan. 7:14.

